# RANGI KAMA MBINU YA USIMBAJI MAANA KATIKA DIWANI YA *RANGI YA ANGA* (KITHAKA WA MBERIA)

NA

LILIAN NZAMBI NDONYE

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI

NOVEMBA 2017

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

…………………………………..                …………………….. 

Lilian Nzambi Ndonye                Tarehe

Mtahiniwa

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia Idara ya Kiswahili.

…………………………                …………………….

Dkt. Zaja Omboga                Tarehe

……………………..                …………

Dkt. Ayub Mukhwana                Tarehe

## TABARUKU

Tasnifu hii nawatabarukia wazazi wangu Bwana Francis Ndonye na Bi. Jane Kavutha kwa kunilea, kunisomesha na wosia wao wa kila mara kuhusu maisha.

Namtabarukia bwanangu mpenzi Charles Omoti, umekuwa mhimili mkubwa katika masomo yangu. Nawatabarukia wanangu Trinidad Kwamboka, Tandi Kerebi na Favor Bosire, wakati mwingine niliwanyima mahitaji muhimu kama mama ili kushughulikia masomo yangu. Mna kila sababu ya kufaulu maishani.

## SHUKRANI

Kazi hii imefanikishwa kutokana na juhudi na ukarimu wa watu kadhaa waliochangia kwa namna moja au nyingine. Naomba kuwataja baadhi yao kwa mawazo na ushauri walionipa mpaka nikafikia kiwango hiki. Kwanza nazitoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya wakati wote niliokuwa nikisoma mpaka nikamaliza hata ingawa nilikumbana na changamoto nyingi. Nawatolea shukrani zangu zisizo kifani wasimamizi wangu, Dkt Zaja Omboga na Dkt Mukhwana kwa ushauri wao na maelekezo mpaka nikamaliza tasnifu hii. Nawashukuru sana kwa muda wenu na kuwajibika kwenu wakati wowote nilipohitaji kuelekezwa. Ningependa pia kuwashukuru wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili ambao mihadhara yao ilikuwa nafasi ya kunishauri kwa njia za kiusomi. Shukrani maalum kwa wahadhiri wafuatao : Prof. Iribe Mwangi, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Rayya, Prof. Mbatia, Prof. John Habwe, Dkt. Leo Sanja, Dkt. Mbuthia, Dkt. Mary Ndung'u, Dkt. Jefwa na Dkt. Jerono.

Hakika si haki kukosa kutoa shukrani zangu kwa wanafunzi wenzangu kwa mchango wao na kunihimiza. Shukrani maalum ziwaendee : Florence Wambui, Claris Uchi, Ray Owalla na Dominic Muinde. Wanafunzi wengine ni pamoja na: Jackline Atieno, Shem Omambia, Githinji, Victor, Rose, Mwita, Nancy, Veronicah, Nina, Christine, Silas, Musamali, Pauline na Okello.

Nawashukuru pia wazazi wangu Bwana Francis Ndonye na mamangu Jane Kavutha. Namshukuru mkutubi wa shule ya upili ya Lari, Bwana Gichogu kwa kuhakikisha nimepata nakala zote nilizozihitaji. Pia namshukuru Bwana Maina, kwa msaada wake usio na kifani kwa kunielekeza namna ya kuchapisha kazi yangu. Namshukuru pia msichana wangu wa kazi za kinyumbani, Damaris Nyaboke, kwa kuhakikisha kuwa kila kitu ki shwari. Mungu akubariki.

# IKISIRI

Tasnifu hii inahusu matumizi ya rangi kama mbinu ya usimbaji maana katika diwani ya *Rangi ya Anga* ya Kithaka wa Mberia. Tumelenga kuchunguza dhima ya rangi kama ilivyotumika katika diwani teule. Vile vile, tulibainisha ishara mbali mbali zinazowakilishwa na rangi tofauti tofauti. Pia, tulilenga kuweka wazi vichochezi vinavyomsukuma mtunzi huyu kutumia rangi katika kazi yake. Haya yote tuliyaweza kwa kutumia nadharia ya semiotiki inayohusu ishara na uashiriaji kwa kuegemea mkondo uliopendekezwa na Charles Pierce. Hii ni kwa sababu kila rangi imetumika kama ishara yenye maana baada ya kutafsiriwa. Nadharia ya semiotiki inashughulika ishara na maana zake kama zinavyotafsiriwa na wanajamii kutokana na mazoea yao ya kuzitumia.

**YALIYOMO**

UNGAMO ........................................................................................ ii
TABARUKU ........................................................................................ iii
IKISIRI ........................................................................................ v
YALIYOMO ........................................................................................ vi
SURA YA KWANZA: ........................................................................................ 1
UTANGULIZI ........................................................................................ 1
1.1 Usuli wa Mada ........................................................................................ 1
1.2 Tatizo la Utafiti ........................................................................................ 7
1.3 Maswali ya Utafiti ........................................................................................ 7
1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................................................ 7
1.5 Sababu za Kuteua Mada ........................................................................................ 8
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........................................................................................ 9
1.7 Yalioandikwa Kuhusu Mada hii. ........................................................................................ 9
1.8 Misingi ya Nadharia ........................................................................................ 14
1.9 Mbinu za Utafiti ........................................................................................ 24
1.9.1 Ukusanyaji wa Data Maktabani ........................................................................................ 25
1.9.2Uteuzi wa Sampuli ........................................................................................ 25
1.9.3 Uwasilishaji wa Data ........................................................................................ 25
1.9.5 Matokeo ........................................................................................ 26
1.9.6 Hitimisho ........................................................................................ 26
SURA YA PILI: ........................................................................................ 27
RANGI NA UMAANA KATIKA DIWANI YA *RANGI YA ANGA* ........................................................................................ 27
2.0 Utangulizi ........................................................................................ 27
2.1 Muhtasari wa Diwani ya Rangi ya Anga ........................................................................................ 27
2.2 Dhana ya Rangi Katika Diwani ya *Rangi ya Anga* ........................................................................................ 28
2.2.1 Mateso ........................................................................................ 32
2.2.2 Mabadiliko ya Mazingira ........................................................................................ 35
2.2.3 Umasikini ........................................................................................ 37
2.2.4 Mkoloni ........................................................................................ 38

2.2.5 Utamaushi ........ 39
2.2.6 Utamaduni ........ 40
2.3 Hitimisho ........ 41
SURA YA TATU: ........ 43
DHIMA YA RANGI KATIKA DIWANI YA *RANGI YA ANGA* ........ 43
3.1 Utangulizi ........ 43
3.1.1 Kusawiri Mazingira ya Binadamu ........ 43
3.1.2 Utambulisho wa Tamaduni za Jamii ........ 48
3.1.3 Kuzua Uhalisia ........ 49
3.1.4 Kutambulisha Tabaka ........ 52
3.2 Hitimisho ........ 53
SURA YA NNE ........ 54
RANGI KAMA KICHOCHEZI CHA MWANDISHI KATIKA DIWANI YA RANGI YA ANGA ........ 54
4.0 Utangulizi ........ 54
4.1 Mazingira ........ 54
4.2 Kutetea Haki za Wanawake ........ 59
4.3 Kuibua Upekee / Ubunifu ........ 60
4.4 Kujaza Pengo la Kiusomi ........ 63
4.5 Kuzindua na Kutahadharisha Jamii ........ 64
4.6 Hitimisho ........ 67
SURA YA TANO ........ 68
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 68
5.1 Utangulizi ........ 68
5.2 Muhtasari ........ 68
5.3 Mapendekezo ........ 68
5.4 Mahitimisho ........ 69
MAREJELEO ........ 70

# SURA YA KWANZA:
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Rangi ni uhalisia wa tamaduni za ulimwengu na ni kigezo muhimu katika kukadiria na kutathmini mitazamo, falsafa na mionoulimwengu ya maisha ya binadamu ya kila siku. Kwa namna mbali mbali, tamaduni za jamii hutawaliwa na matumizi ya rangi anuwai zinazoashiria mambo muhimu kwa jamii husika. Baadhi ya jamii za ulimwengu huitazama rangi kidhahania ilhali jamii nyingine huiona rangi katika misingi ya mahusiano na mambo mseto katika jamii husika. Kwa hivyo, katika msambao mzima wa kuieleza rangi kidhahania au kiutekelezi, rangi tofauti tofauti huwakilisha mambo mbali mbali katika jamii tofauti ulimwenguni. Shughuli nyingi katika jamii huoanishwa na rangi mbali mbali kwa mfano, rangi katika kutabiri au kufasiri matukio, rangi katika kuashiria uzazi hususan jinsia ya mtoto aliyezaliwa, rangi katika matambiko ya michakato ya kumvusha mtoto kutoka hatua moja ya makuzi hadi hatua nyingine, sherehe za harusi, rangi katika michakato ya jinsi tunavyowazika wafu, rangi kama kiashiria cha mahusiano yetu na mifugo au mimea na vile vile rangi katika sherehe za kuvuna mazao shambani, ni miongoni mwa mambo yanayotawaliwa na matumizi ya rangi mbali mbali. Kwa mfano, rangi ya samawati, katika jamii za Ulaya, huashiria uaminifu, usalama na mamlaka. Lakini pia inaweza kuwakilisha upweke, msongo wa mawazo na huzuni. Katika dini ya Hindu, vile vile, rangi ya samawati inahusishwa na Krishna aliyeshirikishwa na upendo na furaha kuu.

Katika jamii ya Wamaasai ya Kenya na Tanzania, rangi ya kijani hutumika kwa maana ya lishe bora na mazao. Pia huwakilisha ardhi ambayo huleta chakula kwao na kwa mifugo wao, vile vile huwashiria haja ya kukinga mipaka yao na kukita mizizi wanakoishi. Katika jamii za Kenya, rangi imesawiriwa kama kigezo chenye umuhimu. Matumizi au maana yake huzingatiwa hasa ili kuhifadhi tamaduni za jamii husika. Kwani, jamii mbali mbali, huadhimisha sherehe mbali mbali za kitamaduni kwa matumizi ya rangi mbali mbali. Kwa mfano, jamii ya Wamaasai, hutumia rangi mbali mbali kusawiri matukio tofauti tofauti katika jamii hiyo. Kwa mfano, rangi nyekundu kuwapaka wapiganaji wao wanapotawazwa kuwa wapiganaji waliohitimu, kumaanisha damu, kuonyesha ukakamavu, nguvu na umoja. Wanaamini kuwa rangi hii huwakinga dhidi ya hatari ya wanyamapori. Rangi nyekundu ndio ambayo imeshamiri katika

mavazi mengi ya Wamaasai hasa shuka wanazojifunika mabegani wanaume kwa wanawake. Kando na rangi nyekundu, Wamaasai pia huwa na rangi nyenginezo ambazo huwashiria maisha na itikadi zao. Kwa mfano, wanaamini kuwa rangi ya samawati ni rangi ya mbingu, ambayo huwaletea maji (mvua), hasa kwa ng'ombe wao ambao wanawasujudu sana kuwa ndio huwapa chakula, mavazi na makao yao. Wamaasai pia huidhamini rangi nyeupe kuwa ni rangi ya usafi na rangi ya maziwa yanayotoka kwa ng'ombe, hivyo weupe wa maziwa huashiria afya kwa sababu ya virutubisho vinavyotokana na maziwa kwa watumizi wake.

Katika dini ya Kikristo, rangi nyeupe huashiria utakatifu na hutumika kueleza mavazi ya malaika na viumbe vitakatifu. Mbali na matumizi ya rangi miongoni mwa jamii mahususi na dini katika nchi mbali mbali, rangi inatumika kitaifa kwa shughuli na utambulisho wa aina mbali mbali. Kwa mfano, takriban katika nchi zote zilizowahi kuwa na mapambano au vita vya ukombozi, bendera za nchi zina rangi nyekundu katika sehemu mojawapo katika bendera hizo. Hii ni kuashiria ukumbusho wa umwagikaji wa damu katika vita vya uhuru.

Katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili kuna kazi zilizotumia dhana ya rangi kuashiria mambo kadha wa kadha. Kwa mfano, katika kitabu cha hadithi fupi: *Damu Nyeusi na hadithi nyingine*, katika hadithi ya *Damu Nyeusi* iliyoandikwa na Ken Walibora, mtunzi ametumia rangi nyeusi ya ngozi ya mhusika Fikirini kurejelea Waafrika na Uafrika kwa jumla. Watu wote walio na rangi nyeusi ya ngozi wamechorwa kuwa ni wajinga, wezi na walio nyuma kimaendeleo. Mtunzi huyu pia ametumia rangi nyeupe kurejelea wazungu, na kuwasawiri kama walio mbele kimaendeleo na wasomi. Katika hali hii mtunzi, anawasilisha mivutano na mapambano yaliyoko kati ya weusi na weupe. Kwa hivyo, kuna uwezekano kwamba, rangi mbali na kuwa uhalisi wa kitamaduni, ni nyenzo, rasilmali na mbinu katika utunzi wa kifasihi katika fasihi ya Kiswahili. Ni nyenzo ambayo imetumiwa katika bunilizi nyingi kusimba dhamira na maudhui mseto kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Katika kitabu cha *Damu Nyeusi* na *Hadithi nyingine,* anwani ya Damu Nyeusi katika diwani hii ya hadithi fupi ya Ken Walibora na Said A. Mohamed ambayo inasawiri rangi ya damu kuwa nyeusi badala ya rangi nyekundu. Mtunzi wa hadithi hii, Ken Walibora, amesimba maana ya rangi nyeusi kwa kuonyesha jinsi Waafrika

walivyonyanyaswa mikononi mwa Wazungu hasa kwa kumwangazia mhusika Fikirini. Rangi nyeusi imetumika kuashiria mateso na matendo maovu ya Wazungu kwa Waafrika.

Kwa kadri inavyodhihirika kutoka katika mukhtasari huu, rangi imesakini katika harakati zote za maisha ya binadamu. Huu ni uhalisi unaojibainisha katika bunilizi simulizi katika jamii nyingi za Kiafrika. Si ajabu kwa hivyo, kwamba katika tamaduni za Afrika, rangi mbali mbali zimeweza kutumika katika tungo za kisimulizi na kiuandishi kuashiria yaliyomo katika masimulizi au vitabu vyenyewe. Historia ya utunzi wa fasihi katika Kiswahili ina ithibati nyingi zinazoonyesha jinsi rangi ilivyosambaa na kuhusianishwa na utunzi wa kibunilizi. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga*, Kithaka ametumia rangi kwa kuihusisha na mambo kadha wa kadha. Hasa katika shairi la '*Zimwi la Theluji'* (uk 49-50) sehemu ya (2) ubeti wa1;

Kwa kunyemelea
Lilikuja zimwi jeupe
Kwanza kwenye upwa
Ambapo upepo
Hupuliza manukato ya chumvi
Kwenye pua za wakazi
Nyanda ambako
Mipeketo na mikungu
Na minazi na mikoko
Na mikanju na mivinje
Huishi kwa amani
Pamoja na korongo
Na kunguru na membe

Mtunzi amehusisha zimwi la theluji na mkoloni kwa kuwa rangi ya ngozi ya mkoloni hutambulika kuwa nyeupe kama ilivyo rangi ya theluji. Hata hivyo katika shairi la '*Wanda'* (uk 31) sehemu ya 2, ubeti wa 7;

Majira ya mvua
Na kijani kibichi
Kikosi cha taya za ng'ombe
Hushambulia nyasi changa

Na kuhujumu miche adimu,
Hutafuna mashina na majani
Na kuwa kizuizi cha chuma
Dhidi ya ngome ya kijani

Kithaka ametumia rangi ya kijani kibichi kwa kuihusisha na athari nzuri za mvua katika mazingira. Nayo rangi nyekundu imetumika (katika shairi hilo) kuashiria hatari zinazoletwa na mvua zikiwepo mmomonyoko wa udongo na mafuriko ambayo husababisha vifo vya watu na mifugo kwa mfano, katika sehemu ya 9 ubeti wa 3 (uk 42)

Vijia vyembamba!
Nyinyi
Wenye mivo mirefu,
Nyinyi
Udhia wa mambo,
Nyinyi
Matokeo ya ushirikiano bahili
Baina ya milolongo ya ng'ombe
Ikifukua ardhi kwa kwato,
Na maji mekundu yakitiririka
Na kuhamisha uhai wa ardhi
Na kuacha mizizi nje
Ishara ya majeraha buka

Neno usimbaji linatokana na neno msimbo ambalo kulingana na Cohan na Shires (1988: 114) wanaeleza kuwa msimbo ni ruwaza ya sheria zisizo tata ambapo ujumbe hugeuzwa kutoka uwakilishaji mmoja hadi mwingine, yaani ishara moja hutumika badala ya ishara nyingine na ambapo kibadala hutokea punde tu uhusiano wa ishara unapotambuliwa. Mgeuzo huu unaokubalika huhusisha kubadilishana maana baina ya mifumo ya ishara. Usimbaji unaweza kudhihirika kwa namna mtunzi wa kazi ya fasihi ya Kiswahili anavyotumia mbinu kama vile picha na taswira kueleza ujumbe wake. Kwa mfano, katika *Nakuruto* yake Clara Momanyi, amejenga picha ya mandhari ya mapango ambayo yana magamba ya kobe yaliyotapakaa, majoka yaliojisuka na yenye rangi mbali mbali mawe yenye maumbo mbali mbali, mifupa mikubwa ya viumbe

wasiofahamika. Mandhari haya yamesimba maana ambayo mtunzi wa riwaya hii anaiwasilisha kwa msomaji. Kwa kuwa yanaashiria matokeo ya uharibifu wa mazingira, ambao unasababisha vifo vya wanyama.

Usimbaji pia unajitokeza katika riwaya kama vile *Msimu wa Vipepeo* na *Harufu ya Mapera* vyake Wamitila. Mtunzi wa riwaya hizi mbili ametumia vipepeo na harufu kusimba ujumbe wake. Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, imesimba maana ya kipepeo kwa kumfananisha mhusika Ndumi na kipepeo kwa kuwa alijua namna ya kupata uhuru wake na kuwasiliana na babake halisi, ambaye alikuwa amenyimwa nafasi ya kuwasiliana naye na mamake Julia na babake wa kambo, Waziri Mkurutu. Hata hivyo dhana ya kipepeo imetumika kuashiria fikra za mhusika Julia ambaye alikuwa ameukimbia umaskini wa mume wa kwanza -Kanda, aliyempenda na kuolewa na Waziri Mkurutu, ambaye alithamini kazi yake kuliko ndoa yao, hasa mkewe. Fikra za Julia kuhusu maisha yake ya sasa na furaha aliyokuwa nayo ilikuwa ya muda na ya kuonyesha usoni tu. Moyoni aliugulika kwa kumtenganisha mwanawe Ndumi na babake mzazi. Riwaya hii imesimba ujumbe wake kwa kutumia *vipepeo*, jinsi diwani ya *Rangi ya Anga* ilivyosheheni matumizi ya rangi mbali mbali kuficha maana ya ujumbe wake. Katika riwaya ya *Harufu ya Mapera,* harufu ya mapera imesimba maana ya rasilmali za wananchi wanaoishi mashambani na ambao hawana namna za kupeleka mazao yao sokoni kwa kukosa miundo misingi. Hivyo waliishia kunusa maendeleo ya wananchi wanaoishi mijini na hawawezi kuyafikia maendeleo kama yale.

Wamitila (2003:116) ameeleza dhana ya msimbo kuwa ni dhana inayotumiwa katika uhakiki kueleza kuwa ni sheria ambazo huwaunganisha wasomaji wa kazi za kifasihi na waandishi wake. Sheria hizi huwawezesha wasomaji hao kuyaelewa mambo mbalimbali katika kazi za kifasihi katika miono inayokaribiana au inayotofautiana kulingana na tajriba zao. Kwa hivyo kulingana na maana wanazozitoa Wamitila, Cohan na mwenzake ni kuwa neno usimbaji ni namna mwandishi anavyoficha na kuwasilisha ujumbe wake kwa kutumia njia fiche za ishara fulani ambayo maana yake hujitokeza pindi tu kibadala chake kinapojitokeza.

Wamitila (2008:17) anasema kuwa maana ya kifasihi si wazi na ni lazima itafutwe ili iweze kubainishwa kwa urahisi. Kwa kutumia mfano wa mwiba, anasema kuwa maana ya kifasihi, huwa si kama mwiba ambao kwa kutumia macho unaweza kujuliana uliko

katika ngozi na kuung'oa. Alichomaanisha ni kuwa ni lazima maana ya kifasihi itafutwe kwa makini ili kuibaini. Baadhi ya njia za kubaini maana ni pamoja na kuitambua misimbo iliyoko na kisha kuifasiri misimbo hiyo kwa misingi ya miktadha ya kiutunzi inayohusika.

Ingawa watunzi wengi wamesimba jumbe zao kwa kutumia vitu mbali mbali kama harufu, vipepeo, picha na taswira kama ilivyo katika diwani ya *Rangi ya Anga*, shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 21), sehemu ya 14, ubeti wa 1;

> Katika vijiji vya shuka nyekundu
> Eneo la shanga shingoni
> Hayawani wenye sare za kijeshi
> Wakitumia hila za zawadi na ahadi
> Huzuza wenye upeo mdogo wa macho
> Wamezewa mate wakoleapo pumbazo
> Wamezapo vyambo walivyotupiwa
> Huporomoshwa chini kwa dhoruba
> Kuzibwa vinywa kwa nguo au vitambara
> Na kuwageuza vyombo vya starehe

Mtunzi amefumba jamii ambazo hutumia vitambaa na shuka za rangi nyekundu huku akiviita vijiji vya shuka nyekundu. Kisha katika mstari wa pili anawatambulisha wenye kutekeleza ubakaji kwa kuwaita wenye sare za kijeshi, kwa maana kuwa wanaotenda matendo haya ni wanajeshi.

Kithaka, ametumia dhana ya rangi kusimba maana ya ujumbe wake katika Diwani ya *Rangi ya Anga.* Mtunzi huyu ameangazia mambo mbali mbali ya kihalisia na kuyahusisha na rangi. Kwa hivyo, ni kutokana na hali hii na jinsi Kithaka alivyopitisha ujumbe wake kwa kutumia rangi katika mashairi huru, ndipo tunakusudia kufanya utafiti kuhusu matumizi ya rangi kama mbinu ya kusimba maana. Hakuna mengi ambayo yamesemwa na wala kuandikiwa na wasomi na wachanganuzi wa fasihi ya Kiswahili kuhusu rangi kama mbinu ya usimbaji maana. Rangi kama dhana au kama mbinu haijashughulikiwa kiusomi katika fasihi ya Kiswahili na ilhali kuna kazi nyingi zilizobuniwa kwa misingi ya rangi au kwa misingi ya kurejelea rangi. Kwa hiyo, ni kutokana na hali hii na jinsi Kithaka alivyopitisha ujumbe wake kwa kutumia rangi

katika mashairi huru, ndipo tunakusudia kufanya utafiti kuhusu matumizi ya rangi kama mbinu ya kusimba maana.

### 1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu ulijishughulisha kubainisha na kuchanganua matumizi ya rangi kama mbinu ya usimbaji maana katika tungo za kifasihi kwa ujumla na katika tungo za mashairi huru, hasa kwa kuangazia diwani ya *Rangi ya Anga* ya Kithaka wa Mberia. Utafiti huu ulichochewa na uhalisi uliopo kwamba kuna kazi katika fasihi ya Kiswahili ambazo zimetumia rangi kama moja ya mbinu za kimsingi katika kusimba maana. Hali kadhalika, utafiti huu ulipania kuhoji kwamba utumiaji wa rangi kama mbinu ya kusimba maana ni mkakati wa kiutekelezi ulio na dhima ya kutahadharisha, kuonya, kusihi, kufunza na kuasa. Vile vile, utafiti huu ulinuia kubaini ni sababu gani zinazowachochea waandishi kutumia rangi kama mbinu ya kusimba maana, hasa inapozingatiwa kwamba jumbe zilizo katika tungo za kifasihi, zinazokusudiwa kujitokeza kutokana na jinsi mbinu za kifasihi zinavyodhamiriwa kuwa kama mbinu za kusanifu na kuzitia nakshi kazi za kiubunifu. Ni muhimu pia, kujaribu kuelewa na kuonyesha kama kuna sababu mahususi za kimaudhui au kifani za kubuni kazi zilizo na jumbe zilizosimbwa kwa rangi.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo:

i) Je, kuna sababu zozote za kimaudhui au kifani zinazochochea matumizi ya rangi kama mbinu ya usimbaji maana katika diwani ya *Rangi ya Anga*?

ii) Je, rangi imetumika kutekeleza majukumu yapi?

iii) Je, rangi imetumika kuibua umaanisho upi katika diwani hii ya *Rangi ya Anga*?

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu katika utafiti wa mada hii ni kuonyesha jinsi rangi ilivyotumika na mtunzi wa diwani ya *Rangi ya Anga* kuashiria mambo mbali mbali ya kudhamira na kimaudhui katika mashairi yote matatu yaliyoko katika diwani teule: *Rangi ya Anga, Wanda* na *Zimwi la Theluji.* Licha ya lengo kuu utafiti huu una malengo mengine mahususi;

i) Kuchunguza majukumu yanayotekelezwa na rangi kama ilivyotumika katika diwani ya *Rangi ya Anga.*

ii) Kubainisha jinsi dhana ya rangi ilivyotumika kuleta umaanisho katika kazi diwani ya *Rangi ya Anga.*

iii) Kutathmini sababu zinazomchochea mtunzi kutumia rangi kama mbinu ya usimbaji ili kuficha maana kiubunifu katika diwani ya *Rangi ya Anga.*

**1.5 Sababu za Kuteua Mada**

Maana katika kazi za kifasihi si jambo lililo wazi linalojibainisha moja kwa moja ila ni jambo ambalo ni sharti maana yake ibainishwe kutokana na usomaji na uchanganuzi makini ndipo maana hiyo iwekwe wazi ili kuwezesha kuelewa kazi yoyote ya kifasihi. Wamitila (2008:17) anasema kuwa maana ya kifasihi si wazi au kitu kinachoweza kubainishwa kwa njia rahisi tu, kwa kutumia mfano wa mwiba, anasema kuwa maana ya kifasihi, si mwiba tu ambao kwa kuangalia ngozi unaweza kujua uko wapi na kuung'oa. Alichomaanisha ni kuwa ni lazima maana ya kifasihi itafutwe kwa makini ili kuibaini. Maana ya kifasihi inaweza kuwa imejikita katika usanifu wa matumizi ya lugha, au katika matumizi bunifu ya picha au taswira mseto alizotumia mtunzi. Kwa hivyo, katika hali ambapo usomaji na uchanganuzi ulidhihirisha matumizi ya picha za uoni au za akilini, ni muhimu kuelewa ujumbe unaowasilishwa na picha husika ndipo kupata maana inayowasilishwa.

Tuliichagua diwani hii ya *Rangi ya Anga* kwa kuwa ni mfano mwafaka wa kazi za kifasihi ambazo zinatumia kipengele cha rangi kusimba maana ya ujumbe wake. Kwa hivyo, tunakusudia kwanza kuitalii kwa makini diwani ya *Rangi ya Anga* ili kubaini msambao wa matumizi ya rangi, aina za rangi zilizotumika, miktadha na mandhari zilizotumika, ubunifu na umakini wa jinsi zilivyotumika, dhamira na maudhui yanayojitokeza kutokana na matumizi hayo ya rangi. Katika hali zote hizi, usomaji na uchanganuzi huu ulikitwa katika nadharia ya semiotiki ili kutuwezesha kubainisha mikakati ya usimbaji kama mikakati ya kiutunzi inavyoweza kuathiri ufasiri na uchunguzi wa maana kama ilivyowasilishwa.

Ingawa kazi mbali mbali za kifasihi zina usimbaji wa aina yake, diwani hii ina ugeni wa kutumia rangi kama ishara ya kufumba maana ya ujumbe wake, kipengee ambacho kinaonekana kupuuzwa au kutoshughulikiwa na wahakiki wengi ikilinganishwa na kazi za kifasihi ambazo zimeandikwa kuhusu rangi. Kwa hivyo tumeona pana haja ya kubaini vichochezi vinavyofanya mtunzi huyu kudhihirisha upekee huu wa kutumia

rangi kama mbinu ya usimbaji. Hivyo, katika kushughulikia nafasi ya rangi kama mbinu ya usimbaji katika shairi huru utafiti huu ulikuwa umechangia haja na dharura ya kushughulikia masuala ibuka katika utunzi wa fasihi ya Kiswahili kwa ujumla na katika diwani ya *Rangi ya Anga* hasa.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika uchanganuzi wa usimbaji maana katika fasihi ya Kiswahili kwa jumla na usimbaji katika ushairi huru hasa. Kimsingi, utafiti huu ulipania kubainisha rangi kama mbinu ya usimbaji, ulihusianisha rangi na dhima yake kidhamira na kimaudhui, ulidhihirisha na kuyaeleza mambo yanayochochea mtunzi kutumia rangi kusimba maana ya ujumbe wake na jinsi usimbaji huo ulivyotumika katika kazi ya *Rangi ya Anga* na athari zake katika fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Tulijikita katika mashairi huru hasa katika kazi ya Kithaka wa Mberia ya *Rangi ya Anga* kupata ithibati na data zilizohitajika katika mjadala huu.

Tulikusudia kubainisha rangi zilizotumiwa na mtunzi kusimba maana aliokusudia kumfikia msomaji na inavyojitokeza katika diwani ya mashairi huru ya *Rangi ya Anga.* Pia tulishughulikia mlingano wa maana ya mtunzi na mazingira ya jamii husika ndio tubaini msukumo wake wa kutumia rangi kama mbinu ya usimbaji. Mifano yote tunayotoa tulijikita katika diwani ya *Rangi ya Anga* ili malengo yetu yasipotoke. Lakini hata hivyo, tulitambua kwamba suala la migogoro na mivutano katika ushairi wa jadi na ushairi huru ni suala linaloweza kujitokeza katika hali kama hii. Hata hivyo, mijadala kama hiyo, ina umuhimu, haikujumuishwa katika utafiti huu.

**1.7 Yalioandikwa Kuhusu Mada hii.**

Mapitio ya machapisho katika sehemu hii yanalenga kuonyesha mambo yafuatayo: taashira, ishara, jazanda, istiara na hata picha au taswira, kwa hivyo tulichunguza kazi ambazo ziliangazia mbinu hizi na zinaoana kwa kiasi na mada yetu. Kwa hivyo, mapitio yaliyojumuishwa hapa ni mapitio yaliyo na mlandano wa masuala ya usimbaji katika fasihi, aina za usimbaji, athari za usimbaji katika fasihi na masuala mengine sawia na hayo. Utafiti huu ulilenga kuonyesha ufaafu na umuhimu wa kutumia rangi katika kuzindua misimamo ya watu, kuonyesha jinsi dhana ya rangi ilivyotumika kuficha maana ya ujumbe. Kubainisha namna dhana ya usimbaji ilivyoelezwa katika fasihi ya

Kiswahili hasa katika mashairi huru na kuonyesha ufaafu wa matumizi ya rangi kama mbinu ya usimbaji.

Suala la ishara lilishughulikiwa katika uchunguzi wa bunilizi za kifasihi. Kwa mfano, kulingana na Griffen (1997) anadai kuwa ishara ni kitu kinachotoa maana kwa kupatana kisifa na kitu kingine moja kwa moja. Griffen alihitimisha kwamba ishara ni kiwakilishi cha kitu kingine kwa kuwa na uhusiano na kitu hicho. Hata hivyo kulingana na Chandler (1931) akimrejelea Pierce, anasema kuwa ishara inaweza kuwa maneno, picha, sauti, harufu, ladha, vitendo au vitu halisi. Msimamo wa Chandler ni kuwa ishara haiwezi kuwa kitu chochote kama hakitatafsiriwa kama ishara. Tunakubaliana na misimamo hii kwani ishara lazima iwe kitu fulani ambacho ni kiwakilisha cha kitu au jambo lingine. Misimamo hii ya Chandler na Griffen ni muhimu katika utafiti huu kwani tulitumia rangi kama mbinu ya usimbaji ili kufumbua ujumbe uliofichwa na mtunzi wa diwani teule.

Uashiriaji una maana pana katika fasihi na hutumiwa kuelezea hali ya matumizi ya ishara, ambapo maneno fulani huashiria vitu vingine. Kulingana na Wamitila (2003), uashiriaji hutumiwa pale ambapo vitu vingine husimama mbadala wa vitu vingine. Tulidai kuwa, uashiriaji hutambulika kwa kuwa na ishara zinazoeleweka kutokana na mazoea ya kuvitumia katika jamii nyingi. Hata hivyo, vitu hivi huhusishwa na sifa fulani. Kwa mfano, msalaba huhusishwa na dini ya Kikristo, kuchomoza kwa jua huhusishwa na kuzaliwa kwa kitu kipya au kupatikana kwa mafanikio, kutua kwa jua huhusishwa na ufu au ukomo wa kitu Utafiti huu ulituongoza katika kuelewa ishara mbali mbali ambazo zilitumiwa katika kazi za kifasihi ili kufumba maana inayowasilishwa. Madai haya ya Wamitila yana mchango mkubwa kwa utafiti huu kwani, yalilenga kujaliza malengo yatu kuwa ili uashiriaji kukamilika lazima kuwepo na ishara na kiashiriwa.

Matumizi ya picha yalifanikiwa kutekeleza jukumu lake kwa kuunganishwa na taswira ambayo huwezekana kwa kutumia maneno yanayochora picha akilini mwa msikilizaji. Mara nyingi taswira huambatana na ishara madai haya ni kulingana na (Kahigi na Mulokozi 1999). Hata hivyo ni vyema kufahamu kuwa, Picha ilitumika kutekeleza usimbaji katika kazi nyingi za kifasihi, usimbaji wa maana katika ushairi umeshughulikiwa kwa kutumia namna inayonasa hisia za wasomaji kwa kupanga

maneno yanayoweza kuunda picha kamili katika akili za wasomaji. Kazi hii inaoana na malengo yetu ya kubaini jinsi usimbaji ulivyowasilishwa kwa kutumia picha na ishara katika kazi za kifasihi.

Usimbaji wa maana ya ujumbe pia unaweza kutumia wanyama kama vile ndege waimbao, malaika na hata wadudu, hii ni mbinu ya taswira ya kiistiari na ishara. Viumbe hawa husukwa kuashiria anachowasilisha mtunzi. Haya ni kwa kuwa, taswira haina budi kuchotwa kutoka katika mazingira yanayozunguka maisha ya wanajamii ambayo wameyaishi na kuyazoea. (Senkoro 1988, Khamis 2004 na Khatib 2011) wanasema kuwa picha katika ushairi huibuka kwa kuchota vitajwa vya viumbe, wanyama, wadudu, matunda na ndege na hata vitu vya thamani kama madini na vitomeo vya utungo fulani wa ushairi unaojitofautisha na mashairi ya jamii nyingine (Khatib Senkoro na Khamis 2011:29). Usimbaji wa ujumbe fulani unaweza kuwa na ishara zisizokadirika kwani mtunzi ana uhuru wa kutumia kitu chochote kutekeleza malengo yake ya kuficha maana. Ingawa kazi hii ilishughulikia ishara kwa kutumia wanyama, utafiti wetu ulitumia rangi kiishara kama mbinu ya kufumba maana. Kazi hii ilitofautiana na malengo ya utafiti wetu kwa kiasi kwa kuwa mada yetu ilijikita katika kuficha maana kwa kutumia rangi.

Ishara zinazoambatanishwa kwenye taswira mara nyingi hufichwa ndani ya tamathali za semi. Ishara ni dhana au mawazo mbali mbali anayotumia msanii wa kazi ya fasihi kuwakilisha vitu, dhana au mawazo mengine. (Abdilatif Abdalla 1973) katika shairi la *Mnazi: vuta n'kuvute* anasawiri hali halisi ya kiuchumi na kisiasa katika jamii zetu za Kiafrika kwa jumla na katika Pwani ya Kenya hasa. Alitumia taswira ya mnazi na walanazi ambayo ni ishara ya mvutano uliopo baina ya Badi na Alii haya ni kulingana na utafiti wa Nyanchama (2004). Kazi hii ni muhimu kwa kuwa ilishughulikia ishara inavyotumiwa kuwasilisha ujumbe fiche kwa wasomaji, na ni kilelezo cha tuliyoyalenga kutimiza katika utafiti huu kwa kuibua maana ya ujumbe wa kazi za kifasihi kwa kutumia ishara.

Rangi mbali mbali katika kazi za kifasihi hutumiwa kuashiria mambo mbali mbali ambayo yana uhalisia katika maisha ya banadamu. Matumizi ya rangi kama vile rangi nyekundu katika kusimba maana kunaleta uhalisia wa hatari, uchungu, huzuni, uhai au kifo. Rangi nyekundu ni ishara ya uhai na vile vile ni ishara ya tahadhari, hatari ya kifo,

kwa kuwa bila damu mwili hauna uhai. Vile vile, rangi nyekundu huashiria jinsi matajiri wanavyoionea fahari hali yao ya utajiri na kuyakanyaga mazulia tajika yaliyo na rangi nyekundu madai haya ni ya Mberia (1997). Tulifikia kuhitimisha kuwa, kila rangi ina jambo inayowakilisha na ndio maana watunzi wengi wa kazi za kifasihi hasa Kithaka Wa Mberia, wanajenga kazi zao kwenye misingi ya uashiriaji. Kazi hii ni muhimu kwa utafiti wetu kwani ina malengo sawa na yetu ya kuonyesha kinachoashiriwa na rangi mbali mbali hasa katika diwani teule ya *Rangi ya Anga*.

Kwa kuwa kila rangi huashiria jambo fulani, kulingana na madai ya Mutiso (1996) anasema kuwa, rangi nyeusi inahusishwa na giza ambalo linahusishwa na mambo kama vile, uchawi, uoga, kushindwa, upweke, msiba, mashetani, wanyama wala watu, mizuka, ujinga miongoni mwa mambo mengine hasi. Madai haya ni ya kweli kwani rangi nyeusi inahusishwa na maovu. Kazi hii ni mfano mzuri katika kutekeleza madhumuni ya tasnifu nzima kwani malengo yake yalioana na ya kazi yetu na kwa hivyo yalitumika kushadidia kauli na mahitimisho ya mijadala yetu. Kwa kuwa tulilenga kuonyesha dhima ya rangi mbali mbali katika diwani ya *Rangi ya Anga.*

Matumizi ya ishara na taashira yametengewa nafasi muhimu katika fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu, mbinu hizi zinapotumika kama tamathali za semi, huwavutia wasomaji wa kazi husika kwa kuwa huonyesha mandhari ya mtunzi wa kazi hiyo ya kifasihi kulingana na (Karanja 2014). Alihitimisha kuwa, kazi isiyo na tamathali za usemi huchosha na kukosa mvuto. Madai haya ya Karanja ni ya kweli kwani kazi yoyote haiwezi kuitwa ya kibunifu kama inakosa tamathali za usemi. Kazi hii ni mfano mwema kwa utafiti wetu kwa kuwa matumizi ya ishara yalituchochea kuendelea kuisoma diwani ya *Rangi ya Anga* ambayo ndio kazi tuliihakiki matumizi yake ya rangi kama ishara ya kufumba maana ya ujumbe.

Ishara pia inaweza kuwa kitu kinachosimamia kitu kingine na kilicho na uhusiano nacho. Kwamba, ishara ni kiashirii na kile kinachosimamia ni kiashiriwa. Kwa mfano, kulingana na Wanyonyi (2011) na Kilanga (2014) rangi nyeusi hutumika kuashiria maombolezo. Ishara pekee haiwezi kudhihirisha na kufafanua kitovu cha maana. Dhana ya ishara imendelezwa kwa maelezo kwamba inawakilisha kitu au hali halisi pasipo lazima ya kufanana. Walihitimisha kwamba, kuna ishara za aina mbali mbali kimataifa. Kwa mfano, njiwa huashiria amani, mawingu meusi huashiria mvua. Watafiti hawa

wamelenga ukweli kwani ishara lazima iwakilishe kitu au uhalisia wa jambo. Utafiti huu unaoana na tulichokusudia kutekeleza katika utafiti wetu hasa ikizingatiwa kuwa unaangazia dhana ya ishara na uashiriaji kwa kutumia nadharia ya saikolojia changanuzi, nasi tulitumia ishara na uashiriaji kama ulivyo katika mapendekezo ya Charles Pierce kwa nadharia ya semiotiki.

Taswira ya kiashiria hutumika kama mbinu ya usimbaji katika kazi za kifasihi kama tamathali za usemi. Kulingana na Too (2011) anadai kuwa uchanganuzi wa mbinu hizi katika kazi za fasihi ya Kiswahili ni muhimu na wa maana zaidi kwa kazi yetu kwani, uchanganuzi wa rangi kama mbinu ya usimbaji umejificha katika tamathali za semi kama vile, ishara, taashira, sitiari na taswira. Kuna aina mbali mbali za sitiari zikiwepo sitiari kuu ambayo hutawala kazi nyingi za kifasihi kutoka mwanzo wa kazi ya kifasihi hadi mwisho na hurudiwarudiwa na kurejelewa na mtunzi mara kwa mara. Kwa mfano, katika shairi la '*Wanda'* (36), sehemu ya 7 ubeti wa 2;

Mvua, ewe rafiki wa uhai
Wewe, matone yatokayo angani
Kuja kukidhi ndoto za viumbe
Wewe, shujaa wa thamani
Ujaye kwa ukarimu adimu,
Mbona umeondoka haraka
Badala ya kuwa mstahamilivu
Na kukaa nasi kwa miezi kadhaa
Ukitukirimu kwa utulivu
Na kututilia ndoto rutuba?

Mshairi ametumia maneno '*mvua rafiki wa uhai'* kuifananisha mvua na apendaye uhai. Tumeegemea kuhitimisha kuwa, sitiari huwasilisha maudhui na dhamira ya kazi ya kifasihi. Sitiari sahili nayo, huwa rahisi kueleweka na wasomaji kwa kuwa hulinganisha vitu viwili moja kwa moja. Vile vile kina sitiari ya usuli ambayo imefungamanishwa na lugha na haiangaliwi kama sitiari tena na watumizi wake. Sitiari hii hupatikana katika utamaduni mahsusi wa watumizi kama vile, akili ni nywele, maisha ni safari na kadhalika.

Sitiari ni mbinu mojawapo za tamathali za usemi na hutumiwa kuwasilisha ujumbe ambao si wa moja kwa moja aidha katika mazungumzo au katika maandishi. Matumizi ya sitiari huchochewa na masuala ya kijamii kwa mfano, neno mikono linahusishwa na wafanyakazi, hii ni kwa sababu, mikono ndio sehemu ya mwili muhimu katika kutenda kazi. Wales (1989) na Levin (1977) wakielezea mawazo ya Aristotle kuhusu sitiari, ambaye aliiona kama mbinu ya kibalagha ambayo imejengwa katika misingi ya mfanano. Alisisitiza kuwa katika sitiari, vitu au hali zinazolinganishwa lazima ziwe na sifa zinazofanana au zinazokaribiana ili kuwezesha msikilizaji au msomaji kuelewa ujumbe unaokusudiwa.

Misimamo ya Too (2011), Wales na Levin (1977) kuhusu sitiari ni ya muhimu kwa utafiti huu kwani usimbaji hujitokeza katika sitiari pia.

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Katika utafiti huu tumetumia nadharia moja ya semiotiki. Nadharia ya semiotiki ni nadharia ambayo inatumiwa kueleza na kushughulikia ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Suala la uashiriaji katika kazi za kifasihi linahusiana na ukweli kwamba kuibuka kwa maana katika kazi ya kiutunzi kunatokana na aina mahususi za matumizi lugha yanayochimuza maana. Uibukaji huo wa maana unaweza kuwa umekitwa katika misingi maalum kama vile kukitwa katika ishara za aina mbali mbali. Kwa misingi hii, semiotiki ni nadharia inayodhamiriwa kumulika jinsi kazi hizo za bunilizi zinavyowasiliana na wasomaji wao. Nadharia hii kimsingi husisitiza masuala ya kifasiri au jinsi sisi kama wasomaji tunavyoifasiri kazi fulani, na vile vile, jinsi usomaji wetu wa kazi za kifasihi mahususi unavyotuchochea kujiuliza kwa nini kazi za kifasihi huwa na maana zilizo nazo kwa wasomaji wake.

Nadharia ya semiotiki ilizuka katika miaka ya 1970 kama nadharia mbadala ya kuchanganua kazi za kifasihi. Hii ilikuwa kama mkakati wa kuondokana na ubanifu wa nadharia za awali kama vile nadharia ya umuundo ambayo ilikuwa imetawala uhakiki na uchanganuzi wa fasihi katika miaka ya 1960. Nadharia hii inashughulika na ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Suala la uashiriaji katika kazi za kifasihi, semiotiki hutumika kumulika jinsi kazi hizo zinavyowasiliana na wasomaji wake. Kwa kuwa nadharia hii husisitiza masuala ya kifasiri au jinsi tunavyoifasiri kazi fulani tu na pia

usomaji wetu wa kazi hizo na kujiuliza kwa nini kazi za kifasihi huwa na maana zilizo nazo kwa wasomaji wake.

Nadharia hii imefaidi kutokana na mawazo ya mwanaisimu wa Ki-swizi, Ferdinand De Saussure (1916), Roland Barthes (1967) pamoja na mwanafalsafa wa Ki-marekani, Charles Pierce (1977). Pierce, anahusishwa na kielelezo cha ishara kilicho na umbo wa pembe tatu. Kwa mujibu wa Pierce, nadharia ya semiotiki imejumuisha sehemu tatu zinazotegemeana: ishara, yambwa na kifasiri. Ishara, kwa mfano, inaweza kuwa neno lililoandikwa, utamkaji fulani. Kwa mfano, mawingu meusi kama ishara ya mvua. Yambwa kwa upande wake, ni kile kinachoashiriwa. Kwa mfano, yambwa ya kinachoandikwa au kusemwa huwa neno linaloambatanishwa au mfano wa mvua huashiriwa na kuwepo kwa mawingu meusi. Kifasiri ndio kipengee muhimu zaidi katika mchango huu wa Pierce kwa nadharia ya semiotiki. Maana ya kifasiri kulingana na Pierce ni kuwa, uashiriaji sio uhusiano wa kijozi kati ya ishara na yambwa. Ishara huashiria kama imefasiriwa. Hivi, hufanya kifasiri kuwa muhimu kwa yaliyomo katika ishara, kwamba maana ya ishara hujitokeza katika ufasiri ambao ishara hiyo inaleta kwa watumiaji wake.

Kwa mujibu wa Pierce, kila ishara huwa na yambwa au kitendwa kinachorejelewa. Kifasiri ni kile kinachochochewa katika akili ya anayefasiri ishara hiyo. Hii inaweza kutazamwa kama ishara ya pili. Kwa mfano, mtu akikuonyesha mbuzi malishoni, ishara ya mbuzi huwa imechochewa na neno ‘mbuzi’ katika lugha ya msemewa au lugha nyingine anayoifahamu akilini mwake. Hiki kitakuwa kifasiri. Wazo la Pierce kuwa ishara haiashirii kwf namna zote na huwa na elementi zinazoweza kuleta athari na ambazo hufanikiwa kwa kutolewa mfano. Kwa mfano, kuwepo kwa fuko katika shamba kutaashiriwa na kuwepo kwa shimo na mchanga. Hilo shimo ni ishara. Hata hivyo sio kila sifa ya shimo hilo huashiria kuwepo kwa fuko, kwa mfano rangi ya mchanga uliotolewa katika lile shimo si sifa ya moja kwa moja ya kuonyesha uwepo wa fuko. Hata hivyo, ukubwa wa shimo hilo hutegemea na kulingana na ukubwa wa fuko aliyelichimba. Sifa hii si muhimu katika kueleza kama fuko yuko shimoni, cha muhimu hapa ni uhusiano wa kiusababishi unaojitokeza baina ya aina ya ukubwa wa mchanga alioutoa kwenye shimo na fuko mwenyewe. Hiki ndicho kionyeshi kikuu cha ishara.

Pierce, katika kueleza yambwa, anasema kuwa kama ilivyo katika ishara, kuwa sio kila sifa huashiria jambo. Kuna baadhi ya sifa za yambwa zinazowezesha ishara kuashiria. Pierce anadai kuwa, uhusiano baina ya yambwa ishara na ishara inayowakilisha ndio husababisha kuwepo kwa yambwa. Yambwa huweka vikwazo au masharti kwa ishara ili kuzuia kufaulu kwa uashiriaji wa yambwa kuliko yambwa kuleta ishara. Yambwa huweka vidhibiti ambavyo ishara lazima iwepo kama itawakilisha yambwa hiyo. Hata hivyo, ni baadhi ya sifa za yambwa ambazo ni muhimu katika mchakato huu wa uashiriaji. Kwa mfano, katika ule mfano wa fuko shambani, yambwa ya ishara hii ni fuko, fuko anasababisha ishara. Ili fuko awe ishara lazima aonekane mwenyewe na asipoonekana hukosa kuwa ishara ya yambwa husika. Ishara zingine za yambwa hii mbali na fuko ni kuwepo kwa kinyesi chake au michoro ya nyayo zake kwenye shamba. Ishara hizi zimekwazwa na uhitaji wa kumwona fuko mwenyewe kwa macho.

Pierce, katika kueleza kifasiri, anaanza kwa kueleza sifa mbili kuu za kifasiri. Kwamba ingawa kifasiri kimebainishwa, kuna uwiano kwamba tutafikia uhusiano wa ishara na yambwa. Ni muhimu kuielewa na kuifasiri au kuendelezwa kwa ishara asilia. Kifasiri huleta ufasiri wa ishara huku ikituruhusu kuwa na uchangamano wa uelewa wa ishara yambwa. Kwamba kifasiri kinafaa kuitwa kitafsiri. Pili, kama ilivyo katika uhusiano wa ishara na yambwa, Pierce anaamini kuwa, uhusiano baina ya ishara na kifasiri ni wa kuchochewa. Kwamba, ishara husababisha kifasiri. Hata hivyo, huu uchochezi si wa kiusababishi lakini ni ishara inayochochea kifasiri kwa kutumia baadhi ya sifa ambazo ishara huashiria yambwa yake kwazo.

Pierce anaeleza ishara kama elementi ambayo imefinyangwa na kufanywa kuwa muhimu zaidi ili kutekeleza kazi ya kuashiria maana. Pierce anatumia maneno kama vile kielekezi, taashira na ishara tanakali. Vipengee hivi vimewekewa msingi na ishara, yambwa na kifasiri. Pierce anaamini kuwa, kila ishara ina misingi inayotegemezwa kwayo ili kufasiriwa kwake kuwezekane. Misingi hiyo huzua aina tatu za ishara: Kielekezi, ishara-tanakali na taashira.

Kielekezi hutumiwa kuelezea uhusiano fulani kati ya ishara na kinachoashiriwa. Kwa mfano, msimulizi katika shairi la '*Rangi ya* Anga' (uk 9) sehemu ya 6 ubeti wa 2,

Kwa masikio matatu
Mawili kichwani

Na la tatu akilini'
Katika cafeteria
Katika chuo kikuu
Nilisikia profesa
Vyeti nyumbani
Fedha mfukoni
Kipara utosini
Ndevu kidevuni
Tabasamu midomoni
Na T-bone viganjani
Akijigamba kwa wenza-
    Nilipoposa, nikachumbia
    Niliyemchumbia, nikamuoa
    Hakuzidi kumi na tatu
    Kwenye mizani ya miaka !

Mtunzi ametumia maelezo ya taswira ya profesa mwenye *T-bone* viganjani kama kielekezi cha uzee.

Ishara -tanakali hutumiwa pale palipo na uhusiano kati ya ishara na kiashiriwa. Kwa mfano, katika diwani husika, katika shairi la '*zimwi la theluji*' (uk 56), sehemu ya 6 ubeti wa 4

LIPU !
Mwako ulilipuka
Mashujaa
Wakauma midomo ya chini
Na kukaza vipaji,
Kati ya visugudi
Na mabega
Misuli ilikakamka
Na kutunisha vilimbili,
Tumbo zilishobea
Mithili ya duma mbioni

Makali ya parange
Yakaigiza umeme angani
Na kwenye mafuvu
Rungu zikafanya kazi kwa ari,
Hewani
Miluzi ya risasi
Ikawa kama sauti za ndege
Wakishindana kuimba mtini
Juu milimani
Mabomu dhidi ya simba
Yalitutuma mithili radi

Mtunzi ametumia tanakali ya sauti LIPU! kuashiria mwako wa ari ya kupigania uhuru wa mashujaa wa Kiafrika kwa nchi zao zilizokuwa mateka wa wakoloni. LIPU! ni ishara- tanakali inayoiga jinsi mlipuko huo ulivyotokea.

Taashira nayo hutumika kuelezea aina ya ishara ambayo huashiria kutokana na matumizi ya kinasibu ya kikawaida tu. Kwa mfano, rangi nyekundu kwenye rinda la mwanafunzi wa kike katika shairi la '*Rangi ya Anga'* (uk 25) sehemu ya 16 ubeti 2,

…Mwanafunzi aliinuka kwa ujasiri
Akasimama mbele ya wenza
Ndipo alipogundua macho kochokocho
Yakinong'onezana kwa ucheshi
Akang'amua lipo lisilo la kawaida,
Alipojikaguakagua kubaini ukweli
Aligunduala kushtua hata asiyeshtuka:
Sare ya shule ilikuwa na baka loevu
Doa, si la rangi ya wino
Si la vumbi la chaki
Bali sura ya baina ya wekundu
Na zambarau iliyokolea

Rangi nyekundu inaashiria rangi ya matatizo ya ukuaji katika mazingira ya kimasikini na vilevile hali ya umasikini inayomweka mtoto-mwanafunzi nyumbani kwa muda wa siku tatu akikosa masomo kila mwezi kwa kukosa hela za kununua vifaa vinavyovaliwa wakati wa hedhi.

Kwa upana, Pierce anasema kuwa nadharia hii imejikita katika uashiriaji, uwakilishaji, urejelezi na maana. Ingawa nadharia za uashiriaji zina historia ndefu, Pierce anaeleza kuwa, ubainifu na ubunifu wa upana na uchangamano wake, katika kushughulikia umuhimu wa kufasiri uashiriaji unaifanya nadharia hii kuwa na uchangamano usioeleweka kwa urahisi kama masomo mengine.

Maelezo haya ya Pierce kuhusu ishara kutegemezwa katika msingi fulani ili kuweza kufasiriwa yanafanana sana na maelezo ya mwanaisimu, Ferdinand De Saussure ambaye aliangalia lugha kama msimbo huku akisisitiza kuwa ishara hazina maana katika upekee wake ila tu zinapofasiriwa katika uhusiano wa ishara na ishara nyingine. Ingawa maelezo ya Ferdinand de Saussure ni muhimu sana katika utafiti huu hatutayaangazia kwani, yamejikita sana katika lugha na isimu ilhali utafiti huu umeegemea upande wa kifasihi hasa ushairi huru. Vipengee vyote vilivyoelezwa na Pierce, tutavitumia kwani vinaegemea katika malengo ya utafiti wetu.

Roland Barthes (1967) kama mwasisi wa nadharia hii amekuwa wa muhimu sana katika kuiwekea nadharia hii msingi. Mawazo yake na ya Julia Kristeva (1977) yameacha athari kubwa katika uhakiki wa ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Barthes anahusishwa na dhana ya msimbo. Aliibuka na neno hili ili kupendekeza namna bora ya kuisoma kazi ya kifasihi au kama wafuasi wake wanavyopenda kusema matini ya kifasihi. Lengo lake lilikuwa kuivunjavunja kazi ya kifasihi katika sehemu ndogo ndogo alizoziita *leksia.* Leksia kulingana na Barthes ni vitengo vidogo vidogo vya kiusomaji ambavyo vina urefu sawa. Kila leksia hudhihirisha misimbo au kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri. Alitambua aina tano kuu za misimbo.

Msimbo wa matukio, unahusu jinsi matukio yanavyofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana ki-athari na ki- sababishi. Kwamba, tukio la kwanza linaendelezwa na kukamilishwa na matukio yanayofuatia katika kazi ya fasihi. Kwa mfano katika diwani

teule, shairi la '*wanda'* (uk 28), sehemu ya 1, ubeti 1,2,3 mtunzi amejenga shairi hili kwa kuonyesha jinsi jua linavyoathiri mazingira ya binadamu na kusababisha madhara mengi kwa watu, mimea na wanyama.

Joto
Linapeperusha bendera
Linatawala kwa maringo
Na kiburi
Linanyanyasa tosi
Na macho
Harara inachokoza kwapa
Na kukereketa migongo

Tazama!
Tazama mayowe kimya
Yakiwayawaya angani
Na kwa ukaidi wa alasiri
Kutisha majani na maua
Na kubabaisha mijusi na nyuki.

Jua!
Ewe jua!
Jua la adhuhuri
Mbona kwa ghadhabu
Unaadhibu chembe za udongo
Kwa halijoto kama ya tanuri?

Jua!
Ewe jua
Jua la wanda za mikwaju
Mimea na samaki
Ndege na wadudu
Na wanyama na mito

Walikutenda ovu gani
Kukuchochea ulipishe kisasi
Kwa ghadhabu pujufu?

Matukio na maelezo ya joto la jua yameendelezwa kwa mfuatano mwema ila msimbo huu hauna mchango wowote katika utafiti wetu kwani hauegemei katika matumizi ya ishara na usimbaji.

Msimbo wa kihemenetiki ni msimbo unaohusu taharuki na unajulikana na baadhi kama msimbo wa kusimulia au kutamba hadithi kwa mfano, katika diwani teule, katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 19) sehemu ya 12, ubeti 12,

Baada ya miezi minne ya machozi
Kiumbe kipya kilifungua mlango
Kikajibwaga kwenye mwanga wa dunia
Mama mkembe na mtoto wa siri
Wakaanza safari ngumu bila ramani
Punde si punde wakaingia kichakani
Wakawa mateka wa michongoma

Baada ya masimulizi haya kuna taharuki ya kutaka kujua yaliyotokea baada ya mama na mtoto kuingia msituni. Hata hivyo, msimbo hauna uhusiano wowote na utafiti wetu.

Msimbo wa kiseme. Neno 'seme' hutumiwa kuelezea elementi nasibishi ya kisemantiki. Hizi ni elementi ambazo zinatuwezesha kupata picha ya mhusika fulani. Msimbo huu unahusiana na jinsi msomaji atakavyoishia kuipata picha ya mhusika fulani. Msimbo huu unahusiana na jinsi msomaji atakavyoishia kuipata picha ya mhusika fulani wa kifasihi. Kwa mfano, katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 22), sehemu ya 14, ubeti 5:

Ghulamu wa jeshi la Malkia wa Uingereza
Kwa bashasha na mikogo ya kibepari
Huendelea kutaanasi katika koloni la jana
Bila kamwe kusimama kizimbani

Kujibu mashtaka ya kulipua maisha,
Huendelea kuishi kwa faraja na kiburi
Bila serikali ya nchi yenye nembo ya simba
Kufunua kinywa na kukamua misuli
Kupambana na mikondo ya giza

Katika ubeti huu, msomaji anapata picha halisi ya mwanajeshi wa umri wa makamo ambaye baada ya kutekeleza uovu hachukuliwi hatua ya kisheria kwa kuwa anatoka katika jeshi la Uingereza. Msimbo huu hausadii katika utafiti huu na hivyo hatuutumii.

Msimbo wa ki-ishara unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavumbua maana za kiishara katika kazi ya kifasihi. Kwa mfano, katika shairi la *'Rangi ya Anga'*(uk 20) sehemu ya 13, ubeti 3;

Baada ya msimu wa ndoto tamu
Kuyoyoma na kufifia machoni
Bila dalili ya tarumbeta na vigelegele
Bila ishara ya ahadi tegemeki
Ndoto ya pete na tumba la viapo
Ilianza kupoteza ukijani-kibichi
Ikaingia umanjano uliokwajuka
Na kisha kijivu kama cha madakata

Maelezo haya yanaibua hali halisi ya kuisha kwa matumaini kwa binti anayetarajia kuolewa. Matumaini yake yanaanza kwa kukolea kama ukijani kibichi kisha kuelekea kuwa umanjano na baadaye matumaini yanapoisha kabisa yanapiga rangi ya kijivu ya madakata. Kwa hivyo kila rangi katika maelezo haya ina ishara mahususi. Msimbo huu tutautumia kwa kiasi kikubwa kwani unahusiana na mada ya utafiti huu kwa kuegemea kwenye usimbaji wenye kutumia ishara kufumba ujumbe.

Msimbo wa kirejelezi unajengwa kutokana na viashirii vya utamaduni unaorejelewa katika kazi inayohusika. Urejelezi huu huunda uhalisi mahsusi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo ya kuipa kazi fulani nguzo ya kitamaduni. Msomaji anaposema anaelewa anachokisema mwandishi huwa anasema

hivyo kutokana na viashirii vya msimbo huu. Kwa mfano, baadhi ya wasomaji wa Kenya wanaweza kuelewa na kung'amua vielekezi vya utamaduni wao katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 23) sehemu 15 ubeti 5;

> Uwezo unapotimu mikononi
> Barubaruhuvumburuka hadi dukani
> Na kujitwalia shanga za rangirangi
> Chombo cha kumvusha kutoka jangwa
> Hadi chemchemi za faraja teule

Ubeti huu una vielekezi vinavyowiana na vile vilivyo katika tamaduni za jamii za kufuga nchini Kenya kwa hivyo msomaji yeyote wa ubeti huu anaelewa mwandishi anachokusudia. Msimbo huu una malengo sawa na ya utafiti huu kwani maelezo mengi katika diwani nzima yanawiana na tamaduni zilizo katika nchi ya Kenya.

Mchango wa Barthes katika nadharia hii, unafaa zaidi kutumika katika usomaji wa nathari, hata hivyo ingawa tumejikita katika usomaji wa mashairi huru, mchango wake katika msimbo wa kiishara na kirejelezi ndio tutakatumia katika utafiti huu.

Hata hivyo mchango wa Langer (1960) hauwezi kuachwa nyumba kwani ni muhimu zaidi katika kuelewa vigezo vingi ambavyo hawa wanasemiotiki wenzake waliweka. Langer alizua nadharia ya semiotiki kwa kuiita nadharia ya ishara na uashiriaji. Alieleza kuwa uashiriaji huwekewa msingi na uelewa na ufahamu wa binadamu kuhusu jambo fulani. Ishara ni vyombo vya kuweka msingi wa vitajwa. Ishara ni kigezo cha ufahamu kinachomwezesha mtu kufikiri kuhusu jambo tofauti na kuwepo wake. Maana ya ishara huwa katika mazungumzo. Langer alieleza kuwa, kila ishara huwa na maana yake na maana hiyo huweza kuwa na maana nyingi kulingana na mahitaji ya jamiina tamaduni za jamii husika. Kwamba ishara huwa na maana inayoashiriwa na maana ya maanainayoashiriwa. Ishara hizi huwa na maana kutokana na miegemeo ya kitamaduni ya wazungumzaji wenyewe.

Nadharia ya semiotiki husisitiza masuala mawili makuu. Kwanza, jinsi tunavyofasiri maana ya matini fulani ya kifasihi. Pili, utathmini kwa nini matini za kifasihi huwa na maana zilizo nazo kwa wasomaji wake. Pia hutathmini dhima ya ishara za kifasihi. Kwa

mfano, wanasemiotiki wanashikilia kuwa kiashiria huweza kuwa kile kile bali kinachoashiriwa au kurejelewa kikawa tofauti. Kwa mfano, kuna tabia za kupeana mvinyo katika jamii za nchi ya Nigeria. Zawadi hii yaweza kuwa na maana ya mapenzi, pongezi, kufariji au kuposa mke na kadhalika, ingawa mvinyo wenyewe ni wa aina tofauti tofauti pia. Nadharia hii pia inatupa vigezo muhimu vya uchanganuzi kama vile, dhana ya kiashirii na kiashiriwa, ishara na uashiriaji ishara za kiurejelezi, kihemenitiki na ishara za kihusika zinazotusaidia kuchanganua kazi za kifasihi.

Ingawa michango ya wataalamu hawa wote ni muhimu katika uhakiki wa kazi za kifasihi, katika utafiti huu tumetumia na kujikita katika mapendekezo na mielekeo ya Charles Pierce na Roland Barthes. Nadharia hii ina mihimili mingi, muhimu na inayooana na malengo ya utafiti huu kulingana na michango ya wanasemiotiki, ndipo tukaamua kuifuata baadhi ya mihimili ya Pierce na ya Roland:

i) Katika mifumo ya semiotiki, ishara huwa na maana nasibishi au maana halisi.

ii) Mielekeo ya Semiotiki huchunguza dhima ya kiashiria.

iii) Kila ishara lazima ifasiriwe ndio itoe maana inayokusudia.

Nadharia hii imetufaa sana katika kuchunguza kipengele cha rangi katika mashairi huru kwenye diwani ya *Rangi ya Anga.* Rangi imetumika kama ishara ambayo inaashiria jambo fulani kwa hivyo tumetumia mchango wa Pierce kuoanisha maana ya ishara ya rangi kama ilivyotumika katika diwani husika.

**1.9 Mbinu za Utafiti**

Katika sehemu hii tulishughulikia njia zote ambazo tulizitumia kupata data iliyotusaidia katika utafiti huu. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na hivyo, tulitambulisha data pamoja na njia ambazo tulitumia mbinu kama vile kusoma tasnifu zinazohusiana na mada yetu, ushauri wa wasimamizi na wahadhiri wengine, ulikuwa wa maana katika kufanikisha mada hii. Katika kusoma tasnifu na makala mbali mbali kwenye majarida, tulipata data inayohusiana na usimbaji, kama vile makala yenye matumizi ya ishara, istiari, jazanda na taswira, dhima ya rangi kama kiwakilishi cha Uafrika, maovu, mapinduzi, mazingira na wakoloni; matumizi ya rangi na njia mbali mbali zinazotumiwa kusimba ujumbe katika kazi za fasihi ya Kiswahili na ushairi huru hasa

### 1.9.1 Ukusanyaji wa Data Maktabani

Katika maktaba tulijikita katika kusoma mashairi yote matatu katika diwani ya *Rangi ya Ang*a ili kupata rangi mbali mbali na matumizi yake, tasnifu zenye mada zinazowiana na mada yetu; kama zile zenye matumizi ya rangi, jazanda, istiari na picha na zilizoangazia usimbaji kwa jumla. Tulisoma makala katika majarida japo si ya kifasihi bali yanahusu mavazi, matambiko na michakato mbali mbali ya kijamii. Tulisoma vitabu vyenye maelezo kuhusu nadharia inayoongoza utafiti huu ya semiotiki kama kitabu cha Umberto Eco (1976) na cha Wamitila (2002). Maelezo ya Eco kuhusu nadharia ya semiotiki yalitupa data ya kutuongoza kuelewa zaidi mihimili ya nadharia nzima semiotiki. Kwa Wamitila tulipata mielekeo ya wanasemiotiki kama vile Roland Barthes na Charles Pierce.

Tulitumia pia mtandao kusoma makala yaliochapishwa katika majarida nyeti na yanayotambuliwa ulimwenguni kutokana na wasomi waliyoyachangia kama vile makala kuhusu jamii ya Wamaasai. Pia tulipata makala ya jinsi fasihi mbali mbali zinavyotumia rangi katika ubunifu wake. Vile vile ushauri wa wasimamizi ulitufaa zaidi. Mambo haya yote yalituwezesha kuelewa zaidi kuhusu mada yetu na kupata habari tosha za kuchangia kwenye utafiti huu.

### 1.9.2 Uteuzi wa Sampuli

Tulitumia mashairi yote matatu yalio katika diwani ya *Rangi ya anga* yake Kithaka wa Mberia yaani shairi la *Rangi ya Anga, Wanda* na *Zimwi la Theluji*. Uteuzi huu wa sampuli ulifanywa kimakusudi na pia kwa kuzingatia kuwa diwani hii ina mashairi matatu pekee kwa hivyo haya yatasadifu kutekeleza malengo ya utafiti huu.

### 1.9.3 Uwasilishaji wa Data

Data kwa ajili ya utafiti wetu ilipatikana katika mashairi matatu yaliyomo katika diwani ya *Rangi ya Anga* yaani: '*Rangi ya anga', 'Wanda' na 'Zimwi la Theluji'*. Kutokana na mashairi haya tulipata data inayoendana na usimbaji katika kila mojawapo ya mashairi haya. Data tuliyopata tuliigawa kutegemea jinsi fani na mbinu za lugha alizozitumia mwandishi zinavyojitokeza katika matumizi yake ya rangi kama mbinu ya usimbaji maana. Tuliyawasilisha matokeo yetu kwa maelezo na ufafanuzi.

### 1.9.4 Uchanganuzi wa Data

Data tuliyoipata katika maktaba tuliichakata kimaelezo. Data tuliyopata maktabani, kwenye mtandao na kutoka kwa wasimamizi wetu imekuwa ya kuridhisha katika utafiti huu. Maelezo tuliyotoa kuhusu data hiyo ni ya kweli kulingana na vile tulivyoyapata kwenye maktaba, mtandao na kwa wasimamizi. Tafsiri za makala ya lugha tofauti tuliifanya kwa umakini ili kuhakikisha kuwa chochote kinachokusudiwa na maana ya ujumbe haijapotoka.

### 1.9.5 Matokeo

Tasnifu hii ilikusudia kuziba pengo la kiusomi kwa kuangazia dhana ya rangi katika mashairi huru, jambo ambalo halijashughulikiwa katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu ulilenga kubainisha dhima ya rangi kwa mujibu wa diwani husika, sababu zinazomchochea mtunzi kutumia rangi katika mashairi yake. Matokeo yake tulitumai yatatumika kama kigezo cha kiusomi katika tafiti zijazo.

### 1.9.6 Hitimisho

Katika sura hii masuala ya kimsingi kuhusu utafiti kwa jumla yalishughulikiwa kama vile dhana ya usimbaji na matumizi yake katika kazi za kifasihi, na hasa usimbaji wa kutumia rangi katika nathari husika. data ya utafiti huu ilipatikana katika maktaba kwa kusoma katika mtandao na vitabu teule. Katika sura ifuatayo, kazi hii ilichunguza na kuhakiki rangi na umaana katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Aidha dhana ya rangi kama ilivyoshughulikiwa katika diwani hii ya *Rangi ya Anga* ilichunguzwa kwa undani huku mambo mbalimbali yanayoashiriwa na rangi hizo yakiwekwa wazi. Kwa mfano, katika shairi la ‘zimwi la theluji’ mtunzi amemfananisha Mkoloni kwa kutumia dhana ya zimwi lenye rangi nyeupe. Kwa kutumia rangi nyeupe, mtunzi amekusudia hili kulingana na rangi ya ngozi ya mkoloni kwani hujulikana kuwa nyeupe ikilinganishwa na waafrika inayotambulika kuwa nyeusi.

# SURA YA PILI

# RANGI NA UMAANA KATIKA DIWANI YA *RANGI YA ANGA*

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia muhtasari wa diwani ya *Rangi ya Anga*kwa kueleza mambo yanayojitokeza katika diwani hii. Tumeeleza jinsi rangi kwa ujumla ilivyotumika katika fasihi simulizi na andishi hasa shairi huru. Vile vile tumeonyesha asili ya ushairi huru na vile vile jinsi mtunzi alivyosuka kazi yake kwa kutumia rangi mbali mbali ili kuzua taswira ya uhalisia wa mambo. Tumeshughulikia dhana ya rangi kama ilivyoangaziwa na mtunzi wa diwani hii, vile vile tumelinganisha rangi inavyotumika na mtunzi wa diwani hii kama ishara ya kusawirihali mbali mbali katika maisha ya binadamu. Mtunzi wa diwani hii amehakikisha kuwa matumizi yake ya rangi yanaoana na uashiriaji wa anachokusudia kukichora katika akili ya msomaji ili kuzua taswira halisi ya ujumbe wake.

## 2.1 Muhtasari wa Diwani ya Rangi ya Anga

*Rangi ya Anga* ni diwani ya mashairi huru ambayo imeandikwa na Kithaka wa Mberia. Imesheheni mashairi matatu yaliyo na maudhui mbalimbali. Mashairi haya yote yameandikwa bila kufuata sheria za arudhi ikizingatiwa kuwa Kithaka wa Mberia ni mmoja wa wanamapinduzi waliounga mkono mashairi yaliyo huru yaani yasiyobanwa na sheria za arudhi, zilizohusu matumizi ya vina, mizani na beti toshelevu. Diwani hii ina shairi la *Rangi ya Anga*, la *Wanda* na la *Zimwi la Theluji*.

Shairi la *'Rangi ya Anga'*ndilo shairi la kwanza katika diwani hii na lina urefu wa sehemu kumi na saba, kila sehemu imesheheni beti zilizojitosheleza kimaudhui na kifani. Shairi hili lina maudhui kuhusu tamaduni, nafasi ya mwanamke katika jamii, ubabedume na umasikini. Katika shairi la *'Rangi ya Anga'*, mtunzi anaangazia hali zinazomkumba mwanamke katika jamii na mtazamo wa mwanamume kuhusu jinsia ya kike. Katika shairi hili pia, mtunzi ameonyesha jinsi jamii inavyomtazama mwanamke au mtoto wa kike kuwa kiumbe dhaifu na mtoto asiyestahiki. Mtunzi ameonyesha jinsi jamii ilivyotunga tamaduni zinazomkandamiza mwanamke na kumnyima haki za kumiliki mali, kujichagulia mume, kusoma, kusema mbele ya wanaume. Vile vile tamaduni hizi zimemlazimu mwanamke kukeketwa na kumsawiri kama kiumbe asiyekuwa na thamani yoyote akilinganishwa na mwanamume. Tamaduni za jamii zimemkweza mwanamume na kumtwaza mwanamke.

Maudhui haya yameonyeshwa kwa kutumia rangi mbali mbali ili kujenga picha inayoonyesha hali halisi katika jamii za Kiafrika. Matumizi ya mbinu za usemi kama vile, taswira na jazanda sawa na istiari yametumika ili kuleta dhana ya usimbaji.

Shairi la pili ni *'Wanda'*. Shairi hili lina urefu wa sehemu kumi na mbili na ambazo zina beti zilizojitosheleza kimaudhui na kifani. Shairi hili lina maudhui ya uchafuzi wa mazingira na athari zake. Mtunzi ametumia rangi kuashiria mabadiliko ya majira na jinsi athari za matendo ya binadamu yanavyoacha ardhi ikiwa katika hali mbaya. Matendo haya ni pamoja na ukataji miti unaosababisha kiangazi na ukosefu wa chakula kwa wanyama na wanadamu, mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na mtindo wa ukulima ambao baadaye unaleta mafuriko na uchafuzi wa mazingira.
Mbinu za tamathali za usemi zimetumika vile vile kwa mfano, mbinu ya istiari, jazanda na taashira.

Shairi la tatu ni la '*Zimwi la Theluji*'. Shairi hili lina urefu wa sehemu tisa ambazo zina beti zilizojitosheleza kimaudhui na kifani. Mtunzi ametumia rangi kwa kuihusisha na hali mbali mbali. Maudhui yaliyomo katika shairi hili nai pamoja na ukoloni, ulaghai na ujasiri. Mtunzi pia anaelezea hali zinazomfika mwananchi na nchi kutokana na ujio wa wakoloni ambao wanazitumia rasilmali za nchi na kujifaidi wao wenyewe na hata kuzipeleka kwao bila kujali athari wanazomwachia mwananchi. Mbinu ya jazanda ndio iliyotumika sana katika shairi hili.

Kwa hivyo diwani hii, imeangazia matukio ambayo yanamwathiri mwanadamu katika maisha yake. Vile vile jinsi mwanadamu anavyoathiri mazingira yake na kusababisha madhara ambayo yanamwacha akiwa katika hatari ya kuangamia. Katika shairi hizi zote mtunzi ametumia rangi kuwakilisha mambo mbali mbali nahata kuchora picha halisi ya uhalisia wa mambo kama yanavyojitokeza.

### 2.2 Dhana ya Rangi Katika Diwani ya *Rangi ya Anga*

Mtunzi wa diwani hii ametumia rangi ili kuwasilisha ujumbe wake kwa njia inayoeleweka na wasomaji wake. Rangi imetumika na mtunzi wa diwani hii kama msingi wa kazi ya yake ili kuashiria mambo mbali mbali kama vile umaskini, ukoloni na hata mabadiliko ya anga yanayochangiwa na uharibifu wa mazingira. Matumizi ya taswira yamefanikisha ubunifu wa mtunzi kuweza kusimba maana ya ujumbe wake.

Taswira mbali mbali zimetumika na mtunzi kuelezea hali tofauti tofauti za mambo yanayojitokeza katika diwani ya *Rangi ya Anga*. Kwa mfano, katika shairi la *'Rangi ya Anga'*, (uk 24, sehemu 16, ubeti2,

> Mwalimu alipomlenga kwa swali
> Akamwagiza ajibu ubaoni,
> Mwanafunzi aliinuka kwa ujasiri
> Akasimama mbele ya wenza
> Ndipo alipogundua macho kochokocho
> Yakinong'onezana kwa ucheshi
> Akang'amua lipo lisilo la kawaida,
> Alipojikaguakagua kubaini ukweli
> Aligundua la kushtua hata asiyeshtuka
> Sare ya shule ilikuwa na baka loevu
> Doa, si la rangi ya wino
> Si la vumbi la chaki
> Bali sura ya baina ya wekundu
> Na zambarau iliyokolea

Mtunzi anaeleza jinsi mwanafunzi darasani anavyoinua mkono kujibu swali la hisabati kisha anapoamka na kuelekea ubaoni ndipo anapogundua kuwa wenzake wanamwangalia na kunong'onezana miongoni mwao. Haya yote ni kwa sababu ya doa kwenye rinda lake ambalo ni la rangi baina ya nyekundu na zambarau iliyokolea. Mtunzi, katika shairi hili ametumia taswira ya katika muktadha wa darasani ili kuwasilisha dhana ya rangi.

Katika shairi la *'wanda'*, (uk 36), sehemu ya saba, ubeti 1,

> Tumevuka daraja ya majira
> Tumeuhama utulivu wa kijani kibichi,
> Huu ni msimu wa ngurumo
> Kwa ari, jualinatutuma angani
> Likibabaisha mimea na viumbe,
> Nalo vumbi lenye maringo

Lina inadi na macho ya msafiri!

Matumizi ya rangi ya kijani kibichi yamedhihirika kwa kuwa, mtunzi anaeleza jinsi msimu wa mvua unavyoleta mabadiliko ya rangi na utulivu wa mazingira. Lakini anaendelea kueleza kuwa wameingia katika majira mengine tofauti ya jua kali na vumbi. Maelezo haya yamejenga taswira maalum kwa msomaji yeyote kuhusu mabadiliko ya mazingira.

Taswira nyingine ni katika shairi la *'wanda'*, (uk 31), sehemu ya 2, ubeti 7,

Majira ya mvua
Na kijani kibichi
Kikosi cha taya za ng'ome
Hushambulia nyasi change
Na kuhujumu miche adimu,
Hutafuna mashina na majani
Na kuwa kizuizi cha chuma
Dhidi ya ngome ya kijani

Matumizi ya rangi ya kijani kibichi yamedhihirika kwa kuwa, mtunzi anaeleza jinsi msimu wa mvua unavyoleta mabadiliko ya rangi na jinsi taya za kikosi cha ng'ombe zinavyoshambulia nyasi changa na kuhujumu miche ambayo si kawaida kupatikana sawa na mashina na majani ya miti. Maelezo haya yamejenga taswira maalum kwa msomaji yeyote.

Mtunzi wa diwani hii ameibua ishara tofauti tofauti kwa kutumia dhana ya rangi. Kulingana na mihimili ya nadharia ya semiotiki, ishara hubaki tu kuwa ishara kama haitatafsiriwa. Kwa mfano, katika shairi la *'Zimwi la theluji'*, (uk 49), sehemu 2 ubeti 1,

Kwa kunyemelea
Lilikuja zimwi jeupe
Kwanza kwenye upwa
Ambapo upepo
Hupuliza manukato ya chumvi

Kwenye pua za wakazi,
Nyanda ambako
Mipeketo na mikungu
Na minazi na mikoko
Na mikanju na mivinje
Huishi kwa amani
Pamoja na korongo
Na kunguru na membe

Mtunzi ametumia ishara ya zimwi jeupe. Ili kuitafsiri ishara hii ya zimwi la theluji, msomaji sharti ailinganishe rangi ya theluji ambayo nyeupe na rangi ya ngozi ya wakoloni ili kupata maana ya ishara hii. Ishara ya zimwi la theluji imetumika kuwakilisha ukoloni ambao uliongozwa na Wazungu ambao rangi ya ngozi yao hutambulika kuwa nyeupe ikilinganishwa na ya Waafrika ambayo huitwa nyeusi. Maana yaishara kulingana na Wamitila (2003) ni ya kufikirika tu. Inaweza kuwa hali ya kitu ambacho kinawakilishwa na ishara hiyo. Uashiriaji ni namna ya kuwasilisha ujumbe kwa kutumia ishara. Mtunzi wa diwani hii ya *Rangi ya Anga*, ametumia ishara ya bakuli kuu ya chumvi kuashiria bahari hasa Bara Hindi kwa kuwa ndiko Wakoloni walikopitia wakiingia Afrika (Shairi la*'Zimwi la Theluji'* (uk 51), sehemu ya 4, ubeti 1,

Lilifika zimwi la theluji
Kutoka upande wa pili
Wa mvumo wa mawimbi
Janga kutoka ng'ambo
Ya bakuli kuu ya chumvi

Mtunzi amefanikisha kazi hii kwa kutumia rangi mbali mbali kuwasilisha ujumbe wake. Amefanya hivi na kukwepa ukawaida ambao umetumika katika kazi nyingi za kifasihi ambazo hazijaleta jambo jipya kama hili la kutumia kigezo cha rangi kusimba maana hasa katika shairi huru. Rangi katika diwani hii teule imetumika kama ishara ya:

### 2.2.1 Mateso

Katika diwani hii dhana ya rangi imetumika kuashiria mambo ambayo yanaonyesha dhuluma na matendo ambayo ni kinyume cha haki za kibinadamu. Kwa mfano, katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 7) sehemu ya 5 ubeti 3,

Kwa masikio yenye huruma
Tumesikia mlio wa makofi
Viganja vikitua mashavuni;
Tumesikia ngumi ngumu
Zikilia juu ya goko na mitulinga
Na kutoa sauti nzitonzito
Kama lwato za ng'ombe
Zikikanyaga mawe njiani
Hujaona uvimbe mweusi
Ukichekelea kwa dhihaka
Juu ya uso au shingo,
Matone ya damu
Yakidondoka puani
Au kutoka kinywani,
Au menoyaliyokuwa imara
Yaliyolegezwa mizizi
Na kutoroka kutoka taya,
Au macho yaliyoigiza nyota
Yakavamiwa na genge la makofi
Yakawa fumbo la dhiki ya ndoa?

Rangi nyeusi kwa kawaida huashiria maovu. Katika ubeti huu, uvimbe mweusi kwenye shingo au uso na matone ya damu, ni ishara ya dhuluma ambazo mwanamke anapata akiwa mikononi mwa mwanamume. Kwa kuwa uvimbe huo unatokana na kuchapwa kwake na mumewe akidai alimlipia mahari na kwamba mwanamke ni kama mtoto na lazima amrudi ili asipoteze njia. Tumechukulia kuwa uvimbe mweusi huu ni ishara ya maovu yanayotekelezwa na wanaume kwa wake wao kwa kuwachapa, ishara ni maneno yanayotumiwa kuelezea vitu ambavyo husimama badala ya vitu vingine, Wamitila (2003).

Katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 21) sehemu ya 14 ubeti 1,

> Katika vijiji vya shuka nyekundu
> Eneo la shanga shingoni
> Hayawani wenye sare za kijeshi
> Wakitumia hila za zawadi na ahadi
> Huzuzua wenye upeo mdogo wa macho
> Wamezewe mate wakoleapo pumbazo
> Wamezapo vyambo walivyotupiwa
> Huporomoshwa chini kwa dhoruba
> Kuzibwa vinywa kwa nguo au vitambara
> Na kuwageuza vyombo vya starehe

Mtunzi ametumia maneno kama vile vijiji vya shuka nyekundu kwa ishara ya kutambulisha jamii fulani ambayo ni maarufu wa kujifunga shuka nyekundu. Hata hivyo rangi nyekundu kwa kawaida huashiria hatari na damu au uhai. Kulingana na ubeti huu kama tujuavyo katika nchi za Afrika mashariki, shuka za rangi nyekundu huhusishwa na jamii za wafugaji. Kwa hivyo ishara ya shuka za rangi nyekundu imetumika kutambulisha jamii tofauti ambazo hufuga wanyama ili kujipa riziki yao.

Rangi nyekundu imetumika hapa kama ishara ya hatari ambayo watoto na wanawake wanapitia wakitagusana na wanaume hasa wanajeshi wanaotakiwa kuwa walinda usalama wao. Wanajeshi hawa wanazua hatari kwa watoto ambao wanatumiwa kama vyombo vya kujistarehesha bila kujali madhara wanayosababisha katika miili ya watoto hao.

Hata hivyo katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 23) sehemu 15 ubeti 5 na 6;

> Uwezo unapotimu mikononi
> Barubaru huvumburuka hadi dukani
> Na kujitwalia shanga za rangirangi
> Chombo cha kumvusha kutoka jangwa
> Hadi chemchemi za faraja teule

Siku iliyopangwa inapowadia
Ghulamu hubeba bunda la shanga
Na huku moyo ukimdundadunda
Humvisha kidosho mikatale shingoni
Kuanzia hii siku tamu kwa mmoja
Siku ya bashasha kwa shababi
Siku ya machozi kwa kimanzi
Kila barubaru ajionapo mhitaji
Kila mwili wake unapootea dhoruba
Ghulamu huacha wenzake mbugani
Na kwa fahari kurejea manyatta
Kusubiri mwangaza kuaga anga
Ndipo atembelee kibanda cha maliwazo
Kwa kanuni zilizodhinishwa na utamaduni
Kudai na kupata faraja ya usiku kucha
Kidosho apende asipende ni mamoja

Mtunzi amejenga dhana ya dhuluma na mateso, katika sehemu hii kwani anatumia ishara ya shanga za rangirangi ambazo mabarubaru wenye ujanja baada ya kumwona binti wanayetaka kuoa, na kuwajulisha wazazi wake humnunulia hizo shanga za rangirangi na kuwavisha wachumba wao siku ya kufunga ndoa. Shanga hizo huwa kama pingu za kumfunga mwanamke kuwa kama maabusu kwani haruhusiwi kutoa maoni kuhusu mchumba wake na wala kujichagulia wa kumuoa au kusema hisia zake kuhusu mambo fulani ambayo anahitajika kushiriki. Baada ya kuvishwa shanga hizo za rangirangi, mwanamke hulazimika kumtimizia kila mwanamume katika jamii nzima, kando na mumewe haja za kimapenzi. Kwani tamaduni za jamii hii zimeidhinisha matendo kama hayo.

Katika shairi la *'Wanda'*, (uk 43) sehemu ya 10 ubeti wa 1,

Ninaposimama
Nyayo zangu
Zimezama hadi ngunyu

Katika machozi mekundu
Moyo wangu
Ukililia uhai

Rangi nyekundu ni inawakilisha hatari, uhai ikizingatiwa kuwa damu ina rangi nyekundu na umwagikaji wa damu kutoka katika mwili huleta kifo. Mshairi ametumia ishara ya machozi mekundu, ambayo yanamtiririka mwathiriwa wa mafuriko ambayo yanatishia kumwangamiza. Mshairi anajuta kuwa machozi yake hayapozi shida za mafuriko yanayomkabili. Katika fungu hili, mshairi anaashiria hatari inayomkabili binadamu kutokana na mafuriko. Ikizingatiwa kuwa rangi nyekundu ni rangi ya damu ambayo ni ishara ya uhai au kifo, machozi mekundu katika muktadha huu yanaashiria hatari ya kifo inayomkabili mhusika.

### 2.2.2 Mabadiliko ya Mazingira

Mabadiliko ya mazingira yanatokea kwa wingi katika shairi la *'Wanda'* (uk 30), sehemu ya 2, ubeti 4,

Kilimo cha lima-hama-lima
Utendaji usioheshimu matuta
Au kutia maanani mche wa mti
Ila unapoahidi matunda
Hicho kilimo cha jadi
Kimepotosha panga
Kushambuliwa mimea
Kwenye kingo za mito
Miinuko ya valima
Na chemchemi adimu

Ubeti huu umeangazia baadhi ya matendo ya binadamu kama vile kilimo cha kulima na kuhama (kilimo kikongwe), kutopanda miti na kudumisha ukataji wake hasa kwenye kingo za mito, miinuko ya milima na kugofua rutuba ya ardhi. Shairi hili linaonyesha jinsi matendo hayo yanavyopelekea matokeo hasi kwa wanadamu yakiwemo mafuriko na kiangazi (jua kali linalowatesa wakulima) kinachoashiriwa na njaa kwa wanyama, ndege na binadamu. Baada ya majira haya ya kiangazi huja majira ya mvua

yanayobadilisha rangi ya mazingira kuwa ya rangi ya kijani kibichi. Kwa mfano, katika (uk 31), sehemu ya 2, ubeti 7

Majira ya mvua
Na kijani kibichi
Kikosi cha taya za ng'ome
Hushambulia nyasi changa
Na kuhujumu miche adimu
Hutafuna mashina na majani
Dhidi ya ngome ya kijani

Mshairi amesawiri mazingira mapya yanayoletwa na kuja kwa mvua, jinsi ng'ombe wanavyofurahia kula nyasi na miche ya mimea ambayo si kawaida kuipata. Hata hivyo kuja kwa mvua hukutana na taka zinakusanyika na kuzuia kupita kwa maji ya mvua hubadilika na kuwa ya rangi nyekundu kuashiria uchafu, na huja kwa kasi na kusababisha mafuriko. Mafuriko hayo huwa hatari kwa wanadamu kwa kuwa hutishia kuua. Majira ya mvua huleta shibe, hujuma na hasara kwa waathiriwa.

Mabadiliko haya pia hutokea katika mito ambapo uchafu wa majira yaliyotangulia husukumwa na kuondolewa na maji yanayoingia. Kwa mfano, katika shairi la *'Wanda'* (uk 35) sehemu ya 5, ubeti 3,

Kwenye mito bila sifa
Ambamo jana alasiri
Maji ya kijani
Yalijikokota kwa uzembe
Yakinung'unikia ukongwe
Mgeni mwekundu
Sasa ananguruma kwa ari
Akivurumisha magogo
Mawe
Mizizi
Mizoga
Shonde

Manyoya
Vigae vya mayai
Na magamba ya nyoka

Kwa kurejelea ubeti huu, mabadiliko ya mazingira yanadhihirishwa na rangi mbali mbali kwani katika mto, maji ya mvua yaliyo na rangi nyekundu husukuma maji ya kitambo ambayo yamepiga rangi ya kijani. Rangi ya kijani na nyekundu katika muktadha huu zimetumika kuleta dhana ya usimbaji. Kulingana na mchago wa Pierce kwa nadharia ya semiotiki alipendekeza kuwa kila ishara ina maana yake. Kwa hivyo, rangi ya kijani ni ishara yauchafu na ukongwe. Rangi nyekundu nayo inawakilisha Hatari kwa kuwa yale maji yaliyoletwa na mvua yalikuwa yanatishia uhai wa wanyama na wanadamu. Ule mwendo wake wa kasi ni ishara tosha kwamba hayakuwa yanajali wanyama kwa vyovyote vile.

### 2.2.3 Umasikini

Umasikini ni hali ya kukosa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, maji safi, mavazi na nyumba. Hali hii ya ufukara inadhihirika katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 25), sehemu ya 16, ubeti wa 5

Baada ya kuuelewa mwili wake mpya
Baada ya kujua kukadiria maumbile
Yalianza mazowea ya kukwepa aibu:
Kila wakati hatari ulipowadia
Alijitenga na ulimwengu wa nje
Nyumbani akaifanya ngome
Kila mwezi, bila kuyumbayumba
Siku tatu za siri nyekundu ya mwili
Masomo yakawa marufuku

Katika ubeti huu, mshairi ametumia rangi nyekundu kuusimba ujumbe wake. Kulingana na maelezo ya Roland kuhusu msimbo wa kiishara ni kwamba msomaji anaweza kuvumbua maana ya ishara katika kazi ya kifasihi. Kwa hivyo maana ya matumizi ya rangi nyekundu katika ubeti huu inaashiria hatari ya umasikini inayosababisha mwanafunzi kukosa vifaa ya kimsingi kukabili matatizo ya ukuaji,

vilevile mwanafunzi kukosa masomo kwa siku tatu kila mwezi ni hatari kwa maisha yake.

### 2.2.4 Mkoloni

Mkoloni ni mtu anayetawala katika nchi isiyo yake na kuwadunisha wenyeji kwa namna mbali mbali. Katika shairi la *'Zimwi la Theluji'*, mtunzi ametumia ishara ya zimwi jeupe. Kwa mfano katika (uk 49), sehemu ya 2 ubeti wa 1:

> Kwa kunyemelea
> Lilikuja zimwi jeupe
> Kwanza kwenye upwa
> Ambapo upepo
> Hupuliza manukato ya chumvi
> Kwenye pua za wakazi,
> Nyanda ambako
> Mipeketo na mikungu
> Na minazi na mikoko
> Na mikanju na mivinje
> Huishi kwa amani
> Pamoja na korongo
> Na kunguru na membe

Kulingana na maelezo yake mtunzi, ni kwamba zimwi jeupe kuja kwenye upwa na mandhari yenye minazi na mikoko ni taswira ya ufuo wa Pwani ya Afrika Mashariki. Zimwi hilo lilisambaa kutoka ufuoni wa bahari hadi maeneo mapya ya bara ambako Maelezo haya yanathibitisha kuwa zimwi jeupe ni ishara inayorejelea ukoloni. Kwa sababu wakoloni waliingia barani Afrika kupitia ufuo wa Bahari ya Hindi na kusambaa katika maeneo mengine ya Bara Afrika.

Mtunzi ametumia neno theluji ambalo kwa kawaida huwa ya rangi nyeupe. Mkoloni amefananishwa na rangi nyeupe kwa kuwa ikilinganishwa na rangi ya ngozi ya Mwafrika, huonekana kuwa nyeupe. Mkoloni amerejelewa kama zimwi kwa kuwa alikuja Afrika kutenda maovu ambayo yalipelekea Bara la Afrika kuwa masikini kwa kunyang'anywa rasilmali zake.

Katika shairi hilo la *'Zimwi la Theluji'* (uk 56), sehemu 6, ubeti wa 4

Anga
Lilitanda wekundu
Na mitini
Kulia bundi

Rangi nyekundu na mlio wa bundi huashiria hatari kulingana mila na desturi za Waafrika. Kwa hivyo, rangi wekundu imetumika kuonyesha hali ya hatari iliyokuwa inawakaribia wakoloni, macho makali kutokana na hasira ya Waafrika waliojitolea kupigania uhuru wao kwa vyovyote vile. Hali ya wekundu katika muktadha huu ni ishara ya kilichokuwa kinadhamiria kutokea katika ya wakoloni na wenyeji wa Afrika. Palizuka kifo na umwagikaji wa damu.

### 2.2.5 Utamaushi

Utamaushi ni hali kukosa matumaini katika maisha na kukosa majibu ya maana ya maisha. Katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 20), sehemu ya 13 ubeti 3,

Baada ya msimu wa ndoto tamu
Kuyoyoma na kufifia machoni
Bila dalili ya tarumbeta na vigelegele
Bila ishara ya ahadi tegemeki
Ndoto ya pete na tumba la viapo
Ilianza kupoteza ukijani-kibichi
Ikaingia umanjano ulikwajuka
Na kisha kijivu kama cha madakata

Mshairi anaeleza kuwa, matumaini ya binti ya kuolewa na mwanamume mlimbwende katika arusi iliyojaa shangwe na vigelegele yaliyoyoma na kufifia kwa kukosa ishara ya ahadi za kuolewa na yeyote. Kwamba ndoto hizo za kuolewa zilianza kupoteza ukijani-kibichi wake ukaingia umanjano uliokwajuka na kisha kijivu kama cha madakata. Hali hii ya utamaushi imesimbwa kwa kutumia rangi ya kijani kibichi, umanjano uliokwajuka na kijivu. Mfuatano wa mabadiliko ya rangi unaonyesha jinsi mwanzoni binti alivyokuwa na matumaini ya hali ya juu kwa kutumia rangi ya kijani

kibichi. Rangi ya kijani kibichi huashiria kunawiri, kustawi na uhai. Matumaini ya binti yalikuwa na yamekolea, kisha matumaini hayo yakachukua rangi ya umanjano uliokwajuka ishara ya kumaanisha ya kwamba binti alianza kuhofia kutoolewa na matumaini kuanza kufifia. Baadaye rangi ya kijivu ambacho ni ishara ya kukosa uhai au kufa kwa matumaini kwanza inapofananishwa na madakata ambayo ni matawi yaliyopukutika kwenye mti na hayana uhai. Mtunzi amechora picha halisi ya uhalisia unaomtawala binadamu yeyote mwenye matumaini ya kutendeka kwa jambo fulani tangu matumaini yakiwa ya juu mpaka jambo hilo linapokosa kutendeka na matumaini kufa.

### 2.2.6 Utamaduni

Utamaduni ni hali ya maisha ya jamii fulani. Hutumika kutambulisha makundi mengi ya jamii mbali mbali. Hii ni kwa sababu kila jamii ina utamaduni wake mahususi usiofanana na wa jamii nyingine. Katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 21), sehemu 14, ubeti 1,

> Katika vijiji vya shuka nyekundu
> Eneo la shanga shingoni
> Hayawani wenye sare za kijeshi
> Wakitumia hila za zawadi na ahadi
> Huzuzua wenye upeo mdogo wa macho
> Wamezewe mate wakoleapo pumbazo
> Wamezapo vyambo walivyotupiwa
> Huporomoshwa chini kwa dhoruba
> Kuzibwa vinywa kwa nguo au vitambara
> Na kuwageuza vyombo vya starehe

Mtunzi ametumia maneno kama vile 'vijiji vya shuka nyekundu na shanga shingoni' maelezo haya yanafanana na ya jamii ya jamii za wafugaji nchini Kenya. Hii ni kwa sababu, ili kujua utamaduni wa jamii fulani na kuitofautisha na jamii nyingine, mambo ya kuzingatia huwa chakula, mavazi na nyumba. Kulingana na shairi hili, matumizi ya shuka ya rangi nyekundu imetumika kusimba uhalisi wa jamii hii. Rangi nyekundu kwa shuka wanazojifunika wenyeji wa jamii za wafugaji. Kwa kuwa rangi nyekundu kwao ni ishara ya ukakamavu, nguvu na umoja. Wao huamini kuwa rangi nyekundu

huwakinga wapiganaji wao kutokana na hatari za wanyamapori. Rangi hii hutumika sana kwa wapiganaji waliohitimu kutawazwa kuwa wapiganaji halisi.

Katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 23) sehemu ya 15, ubeti 4 na 5),

Ombi linapendeza masikio masikivu
Bila banati kuulizwa msimamo
Bila kujali kama kibali cha wazazi
Kitaufanya moyo wake kuwaa kwa furaha
Au kufa ganzi kwa kumbo la majonzi
Ghulamu huanza mikakati kabambe
Kutafuta hadi kupata uwezo wa darahima
Kununulia shanga za rangiran

Uwezo unapotimu mikononi
Barubaru huvumburuka hadi dukani
Na kujitwalia shanga za rangirangi
Chombo cha kumvusha kutoka jangwa
Hadi chemchemi za faraja teule

Mshairi anaeleza kuwa, katika jamii hii, mwanaume aliyehitimu umri wa kuoa, baada ya kuwaambia na kuwasikiliza wazazi wa binti hununua shanga za rangirangi ili kumwoza binti pindi siku ya arusi inapowadia. Shanga hizi za rangirangi ni ishara inayotumiwa kusheheni maana zaidi ya moja kwani ni daraja inayotumiwa na wanaume kama kigezo cha kuwavusha katika ukapera hadi kwenye chemchemi za ndoa. Pia shanga hizi za rangirangi hutumiwa kama pingu za maisha kwa binti na huwa ishara kuwa kila mwanaume atatumia kama kigezo cha kutimizia haja zake hii yote ni kwa sababu jamii imeidhinisha hilo. Shanga hizi rangirangi ni ishara ya kilio kwa binti na ishara ya furaha kwa wanaume.

### 2.3 Hitimisho

Mashairi ya diwani ya *Rangi ya Anga* yamefaulu katika kujenga kazi kwa kutumia rangi kama ishara inayowakilisha mambo mbali mbali kama vile; umasikini, mateso, utamaduni, kutamauka, mkoloni na mabadiliko ya mazingira. Mambo haya yote

yamejengeka kama ishara inayowakilishwa na rangi mahususi. Kila rangi ina jukumu maalumu inaweza kutumika kama ishara ya jambo fulani au pia kujenga taswira fulani katika akili ya msikilizaji au hata msomaji wa kazi yoyote ya fasihi.

Katika sura ifuatayo tulichunguza dhima ya rangi na jinsi rangi ilitumika kutekeleza majukumu mbalimbali katika diwani ya *Rangi ya Anga.*

# SURA YA TATU

# DHIMA YA RANGI KATIKA DIWANI YA *RANGI YA ANGA*

## 3.1 Utangulizi

Katika sura, hii tumeangazia dhima ya rangi. Matumizi ya rangi katika kazi za kifasihi ni jambo la kijadi ikizingatiwa kuwa matumizi ya rangi yalipatikana katika hadithi za kwanza tangu kuumbwa kwa binadamu. Matumizi haya ya rangi yalikusudia kujenga picha za wahusika wa hadithini, mandhari na matukio. Lugha ya kifasihi hutumia mbinu za kiishara aidha za kuzungumza au za kuandikwa. Matumizi ya rangi katika fasihi kama ishara huleta maana yenye maana ya ndani kwa maneno yaliyotumika ambayo hutumika kubadilisha maneno yaliyoandikwa kuwa kama chombo chenye nguvu katika kuwasilisha maana ya ujumbe uliokusudiwa. Ili msomaji aelewe maana inayowasilishwa na rangi fulani ipasavyo, lazima awe na ujuzi wa rangi husika katika maisha yake. Hii ndio maana wasomaji huwa na tafsiri tofauti kuhusu kazi mbalimbali za kifasihi.

Kwa kuzingatia kuwa rangi ina matumizi tofauti tofauti katika maisha ya binadamu na ni kwa sababu ya matumizi haya ya rangi katika maisha ya kila siku ndiyo inayofanya watunzi hasa mtunzi wa diwani ya *Rangi ya Anga*, Kithaka wa Mberia, kutumia rangi katika utunzi wao. Jinsi fasihi inavyotumia lugha kama malighafi yake ili kuwasilisha ujumbe wake kwa ufundi, fasihi kama sanaa huweza kupambwa kwa kutumia rangi mbalimbali kuwasilisha ujumbe wake kwa namna inayoakisi uhalisia wa mambo.Rangi katika diwani ya *Rangi ya Anga* imetumika kutekeleza majukumu kama vile: kutambulisha jamii kulingana na maelezo ya mtunzi kwa kutumia rangi inayohusishwa na jamii mahsusi, kuonyesha uhalisia wa mazingira anamoishi binadamu kwa kuchora picha maalumu ya uhalisia wa mambo yanayomzunguka binadamu, kueleza tamaduni za jamii kwa kuzihusisha na shughuli zao za kila siku.

### 3.1.1 Kusawiri Mazingira ya Binadamu

Kila binadamu huishi katika mazingira yake. Mazingira ni jumla ya vitu vinavyomzunguka bainadamu anapoishi kila siku. Mtunzi wa diwani ya *Rangi ya Anga* amechora mazingira ya binadamu katika shairi la *'Wanda'* kwa kuonyeha jinsi binadamu anavyoathiri mazingira yake kwa kujua au kutojua. Athari zozote hasi katika mazingira humrudia binadamu kwa ubaya na kutishia kifo. Kwa mfano, katika shairi la

'*Wanda'* mtunzi anatanguliza shairi hilo kwa kuonyesha jinsi joto linavyozitesa tosi na macho na kukereketa migongo na vile vile kutishia uhai wa mimea kwa kukausha maua na majani. Jua nalo linaadhibu chembe za udongo. Wanyama kama vile samaki, ndege na wadudu wanateswa kwa kuchomwa na jua kali. Katika shairi la *'Wanda'*, (uk 32) sehemu ya 2, ubeti wa 8,

Wakati wa kiangazi
Na mazigazi
Ndimi kakamavu za mifugo
Huzoazoa madakata ardhini
Na kunyima miti lishe
Hudhoofisha ngao ya ardhi
Na kuinyima uimara
Wa kuhimili mashambulizi
Ya matone buka ya mvua
Na mtiririko wa fujo
Wa maji mekundu

Mtunzi anaeleza jinsi mifugo walivyo adui wa maumbile kwani huathiri mazingira ya binadamu, hayo madhara yote yanamrudia yeye (binadamu) na vizazi vijavyo. Mtunzi ameendelea kueleza uzito wa madhara ya binadamu kwa mazingira kwani fujo ya maji ya mvua haiwezi kubakisha uhai wa chochote. Amelinganisha athari za maji ya mvua kwa kuyaita maji mekundu. Rangi nyekundu katika muktadha huu ni ishara ya hatari na hata kifo hasa kwa wanyama na binadamu kwa sababu ya mafuriko.

Wakati wa kiangazi, ng'ombe hawa hukusanya madakata (rangi ya kijivu yaani hayana uhai) kwenye ardhi na kunyima miti lishe na hivyo kuinyima uhai na uimara wa kuhimili mashambilizi ya mtiririko wa fujo wa matone ya mvua yenye maji mekundu. Huu wekundu ni matokeo ya kuchanganyika kwa maji na mchanga unaobebwa na maji na kuacha mawe wazi. Baada ya jua na mvua, huja upepo mkali ambao uwacha kama umebeba kila kitu kama vile paa za nyumba, udongo na kuzipeperusha juu kwa fujo kama pia nyekundu.

Athari za kilimo cha jadi cha kisichotumia matuta ambayo huzuia mmomomonyoko wa udongo, kuharibiwa kwa mimea na kuondoshwa kwa kingo za mito, miinuko ya milima na chemchemi za maji. Kilimo hiki hugofua rutuba na kuuondoa urembo wa mazingira kwa kusababisha mmomonyoko wa udongo na kuacha mawe wazi. Bali wakati mvua inaponyesha, mazingira haya hubadilika na kuwa na ukijani kibichi ambapo taya za ng'ombe hushambulia nyasi, miche, matawi na mashina ambayo ni adimu sana kupatikana. Hata hivyo huzuiwa na mawe na mchanga dhidi ya kula nyasi kwa kufuata rangi yake ya kijani. Kwa mfano, katika (uk 31), sehemu ya 2, ubeti 7;

Majira ya mvua
Na kijani kibichi
Kikosi cha taya za ng'ome
Hushambulia nyasi changa
Na kuhujumu miche adimu
Hutafuna mashina na majani
Dhidi ya ngome ya kijani

Rangi ya kijani katika kifungu hiki inaonyesha mabadiliko mazuri yanayoletwa na mvua kwa mazingira ya binadamu. Kwa kawaida rangi ya kijani huashiria uhai na ustawi kwa kuwa kunaponyesha, hiyo ndio rangi hutawala katika mazingira na huwa ishara ya shibe kwa kuwa wakulima huvuna mazao yao ya ukulima.

Majira ya mvua huja kwa kutandwa kwa mawingu, utomvu mwekundu kujitokeza. Majira haya huwashiria shibe, ukarimu, hujuma na hasara. Kwa kuwa kabla ya majira haya kulikuwa na mchanga mweupe kuonyesha kuwa hakukuwa na mchanga unaoweza kusitiri kugofuliwa kwa udongo na maji ya mvua. Kwa mfano, katika (uk 34), sehemu ya 5, ubeti 1 na 2:

Leo mawingu yametanda
Na kupamba turubai ya alasiri
Kwa utomvu mwekundu-
Yametimu majira mapya
Majira ya ukarimu na shibe

Na hujuma na hasara

Ambamo mkazi wa jana
Alikuwa mchanga mweupe
Au miamba myeusi tititi,
Au kijivu au zambarau
Ikitulia bila wasiwasi,
Sasa maji ya hisia mekundu
Yanatiririka kwa fujo
Mto uliokuwa ukilia kwa kiu-
Umekunywa maji ukakinai
Sasa, badala ya kuwa na kikuku
Unashindana na mito isiyokauka
Kuona ni nani mwenda kasi zaidi

Maji ya mvua ya hisia nyekundu ni ishara ya usimbaji ya kufumba maana ya kutiririka kwa fujo na kutishia maisha ya binadamu kwa mafuriko yanayobeba mifugo, nyumba na binadamu wenyewe, kwa kuwa wekundu huashiria hatari. Hatari hii inaweza kuwa ya kifo kwa mifugo na binadamu.

Mtunzi wa shairi hili la *'Wanda'* ametumia rangi kuonyesha mabadiliko ya mazingira ya binadamu kwa kufuata majira na misimu mbalimbali. Kila msimu umechorwa kuwakilishwa na rangi mahususi. Kwa mfano, katika (uk 36), sehemu ya 7, ubeti 1,

Tumevuka tena daraja ya majira
Tumeuhama utulivu wa kijani kibichi,
Huu ni msimu wa ngurumo
Kwa ari, jua linatutuma angani
Likibabaisha mimea na viumbe
Nalo vumbi lenye maringo
Lina inadi na macho ya msafiri

Majira ya mvua yanatambuliwa kama majira ya utulivu wa kijani kibichi. Rangi hii katika sehemu hiyo hiyo ya 7 na ubeti wa 6 na 7,

Ewe kijani-kibichi
Wewe nembo ya uhai,
Nakuotea daima,
Wewe
Ishara ya uzima
Wewe,
Kipenzi cha moyo

Mvua, ewe mvua, tamanio
Wewe
Mganga mahiri
Ungehitaji kulipwa kwa dhahabu
Au kwa almasi, lulu au feruzi
Ili kukwangu hii shaka lowezi
Itokomee kutoka nyoyo za wakulima
Kwa kuinua bendera ya kijani kibichi
Na kuipeperusha kwa fahari
Kwenye mlingotiwa ua wa maisha

Mtunzi anaifananisha rangi ya kijani kibichi na uhai; ishara ya uzima. Mtunzi anaisifu mvua na kuiita kipenzi cha wengi kwani hakuna anayeweza kukosewa na mvua. Kwa hivyo, kama ilivyo katika misingi ya nadharia ya semiotiki kwamba lazima kila ishara ifasiriwe na msomaji, ishara ya rangi ya kijani kibichi ni ishara ya utulivu na uhai katika mzingira ya binadamu. Hali hii ya kuwa na rangi ya kijani kibichi huletwa na kuwepo kwa mvua.

Katika shairi la *'wanda'* (uk 43), sehemu ya 10, ubeti wa 1;

Ninaposimama
Nyayo zangu
Zimezama hadi ngunyu
Katika machozi mekundu,
Moyo wangu
Ukililia uhai

Mtunzi anaeleza jinsi athari za ukataji miti na kubebwa kwa udongo kulivyoleta mafuriko. Mwathiriwa analilia uhai wake kwani mafuriko yanatishia kummaliza pamoja na nyumba yake. Kilio cha machozi mekundu ni ishara ya hatari inayomkabili msimulizi na kutishia kumwuua (kifo).

### 3.1.2 Utambulisho wa Tamaduni za Jamii

Kila jamii huwa na tamaduni zake tofauti na jamii nyingine. Jamii hutambulishwa pia na shughuli zake za kila siku kama vile ukulima na ufugaji, lugha, mavazi na mkao wa nyumba zao. Tamaduni za jamii moja hazilingani na za jamii nyingine kwani kila jamii huwa na shughuli tofauti na nyingine. Katika shairi la *'Rangi la Anga'*, (uk 21), sehemu 14, ubeti 1,

> Katika vijiji vya shuka nyekundu
> Eneo la shanga shingoni
> Hayawani wenye sare za kijeshi
> Wakitumia hila za zawadi na ahadi
> Huzuzua wenye upeo mdogo wa macho
> Wamezewe mate wakoleapo pumbazo
> Wamezapo vyambo walivyotupiwa
> Huporomoshwa chini kwa dhoruba
> Kuzibwa vinywa kwa nguo au vitambara
> Na kuwageuza vyombo vya starehe

Mtunzi ameeleza jinsi vijiji vya shuka nyekundu na wenyeji wake wanatumia shanga shingoni, haya ni maelezo yanayooana na ya jamii za wafugaji barani Afrika, kwa kuwa wanatumia shanga kama pambo na kwa kutekeleza majukumu mengine kama vile kuposea msichana. Matumizi ya rangi nyekundu ni ishara yao ya utambulisho. Kwani kulingana na imani zao ni kwamba, rangi nyekundu huwakinga kutokana na hatari za wanyama pori.

Katika mtunzi anajenga taswira ya jamii ya sime na kanga, mikuki na shanga ambazo hutumika sana na vijana wa jamii mahususi. Katika maelezo haya mtunzi anatambulisha jamii ambazo hutumia vifaa hivi katika shughuli mbali mbali. Jamii

inayotambulishwa hapa na mtunzi ni jamii zinazofuga wanyama kama vile ng'ombe. Katika jamii hii, wanaume huchagua binti wa kuoa na kumposea kwa wazazi wake bila ya idhini ya binti huyo. Binti huja kuozwa kwa mwanaume asiyemjua wala kumpenda. Kijana huyu hununua shanga za rangirangi ambazo hutumia kama zawadi kwa binti-bibi harusi katika sherehe za kitamaduni za kuoa. Katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 23) sehemu ya 15, ubeti 4 na 5),

> Ombi linapendeza masikio masikivu
> Bila banati kuulizwa msimamo
> Bila kujali kama kibali cha wazazi
> Kitaufanya moyo wake kuwaa kwa furaha
> Au kufa ganzi kwa kumbo la majonzi
> Ghulamu huanza mikakati kabambe
> Kutafuta hadi kupata uwezo wa darahima
> Kununulia shanga za rangiran
>
> Uwezo unapotimu mikononi
> Barubaru huvumburuka hadi dukani
> Na kujitwalia shanga za rangirangi
> Chombo cha kumvusha kutoka jangwa
> Hadi chemchemi za faraja teule

Katika utamaduni wa jamii hizi, shanga za rangirangi ni ishara ya kusimba pingu za Maisha. Kwani, mwanamke hufishwa shanga hizo kama ishara ya kuwa mke wa jamii nzima. Jambo ambalo limeruhusiwa na jamii nzima.

### 3.1.3 Kuzua Uhalisia

Uhalisia ni hali kuonyesha mambo na ukweli kama unavyojitokeza; mara nyingi uhalisia huwa tofauti na jinsi binadamu anavyotarajia na hushindwa kuupokea. Kwa mfano katika shairi la *'Zimwi la Theluji'*, mtunzi ametanguliza anwani ya shairi hili kwa kuiitwa '*Zimwi la Theluji'*. Anwani hii inajenga taswira ya kiumbe wa kutisha ambaye ana umbo la barafu. Theluji hujulikana kuwa na rangi nyeupe kwa hivyo, weupe huu unalinganishwa na rangi ya ngozi wakoloni ambao kama tujuavyo walikuja barani Afrika kutawala na kuchukua rasilmali za waafrika. Matendo ya zimwi lolote

huwa hayapendelei binadamu kwa hivyo kila jambo litendwalo na zimwi huathiri mwanadamu kwa uovu wake.

Mtunzi anaeleza kuwa zimwi lilikuja kwenye upwa wa bahari na likasambaa mpaka maeneo ya nchi kavu ambako nyani na tumbili hurukaruka kwenye tanzu. Jinsi wakati ulivyoenda ndivyo zimwi lilivyoenea kote na kusambaza athari zake.

Baada ya miaka kadhaa Wakoloni walifaulu kushika usukani wa rasilmali za bara nzima walihakikisha kuwa wamekita mizizi kweli kwani Mwafrika kujiokoa kutokana na Mkoloni angemwaga jasho au hata damu. Waafrika walipogundua haya walifanya mikutano na kujitayarisha na kujitoa mhanga kuokoa bara lao, kutoka kwa mikono ya mkoloni. Katika shairi la *'Zimwi la Theluji'*sehemu ya 6, ubeti wa 3.

> Anga
> Lilitanda wekundu
> Na mitini
> Kulia bundi

Mtunzi anachora taswira ya jinsi anga lilitanda wekundu na bundi kulia mitini. Mlio wa bundi ni ishara ya bahati mbaya na kwamba kuna jambo ambalo halitaenda kama lilivyotarajiwa. Nayo hali ya wekundu ni ishara ya hatari au umwagikaji wa damu. Damu huashiria uhai na kifo pia. Matokeo ya mapigano haya yalikuwa kupanda kwa idadi ya wajane na mayatima na wakoloni walirejea kwao.

Katika kuonyesha uhalisia, mtunzi wa diwani ya Rangi ya Anga amechora taswira za aina tofauti tofauti. Kwa mfano, kwa kutumia anwani ya ya shairi ya *'Zimwi la theluji'*amejenga taswira ya kiishara. Taswira ya kiishara ni picha iliyo na maana nyingine ya ziada. Maana yake ni zaidi ya maana ya maneno yaliyotumiwa katika ukawaida wake. Maneno Zimwi la Theluji si kiumbe wa kutisha mwenye umbo la barafu tu bali kulingana na maelezo ya mtunzi anatoa maelezo ya Mkoloni. Kwa hivyo zimwi la theluji ni ishara yenye maana ya mkoloni.

Katika shairi la *'Rangi ya Anga'*, *'Rangi ya Anga'* (uk 7) sehemu ya 5 ubeti 3,

> Kwa masikio yenye huruma

Tumesikia mlio wa makofi
Viganja vikitua mashavuni;
Tumesikia ngumi ngumu
Zikilia juu ya goko na mitulinga
Na kutoa sauti nzitonzito
Kama lwato za ng'ombe
Zikikanyaga mawe njiani
Hujaona uvimbe mweusi
Ukichekelea kwa dhihaka
Juu ya uso au shingo,
Matone ya damu
Yakidondoka puani
Au kutoka kinywani,
Au meno yaliyokuwa imara
Yaliyolegezwa mizizi
Na kutoroka kutoka taya,
Au macho yaliyoigiza nyota
Yakavamiwa na genge la makofi
Yakawa fumbo la dhiki ya ndoa?

Mtunzi amejenga picha ya mwanamke anayedhulumiwa kwa kusema kuwa baada ya kusikia mlio wa makofi na viganja mashavuni na ngumi ngumu zikilia kwenye mitulinga. Kisha uvimbe mweusi ambao uko usoni au shingoni na matone ya damu yakidondoka puani au kinywani au meno yaliyokuwa imara kuwa na mizizi legevu. Taswira inayojijenga hapa ni ya uhalisia ambao wanawake wanapitia mikononi mwa wanaume. Rangi nyeusi ni ishara iliyotumika kufumba mathila mwanamke aliyofanyiwa na mumewe. Kwa kawaida rangi nyeusi huchukuliwa kuwashiria mambo mabaya kama vile uchawi, kifo; Katika muktadha huu, rangi nyeusi inaashiria maumivu na maovu yanayotendewa wanawake katika ndoa.

Katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 20), sehemu ya 13 ubeti 3,

Baada ya msimu wa ndoto tamu
Kuyoyoma na kufifia machoni

Bila dalili ya tarumbeta na vigelegele
Bila ishara ya ahadi tegemeki
Ndoto ya pete na tumba la viapo
Ilianza kupoteza ukijani-kibichi
Ikaingia umanjano ulikwajuka
Na kisha kijivu kama cha madakata

### 3.1.4 Kutambulisha Tabaka

Utabaka ni mfumo wa kijamii unaowagawa watu kwenye makundi kutegemea uwezo wao wa kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kila kundi ambalo hugawika kutoka kwa jamii pana kulingana na uwezo wake wa kiuchumi, utambulika kama tabaka.

Katika shairi la*'Rangi ya Anga'* (uk 21) sehemu ya 14, ubeti 1,

Katika vijiji vya shuka nyekundu
Eneo la shanga shingoni
Hayawani wenye sare za kijeshi
Wakitumia hila za zawadi na ahadi
Huzuzua wenye upeo mdogo wa macho
Wamezewe mate wakoleapo pumbazo
Wamezapo vyambo walivyotupiwa
Huporomoshwa chini kwa dhoruba
Kuzibwa vinywa kwa nguo au vitambara
Na kuwageuza vyombo vya starehe

Mtunzi ametumia maelezo ya hayawani wenye sare za jeshi la Malkia wa Uingereza kama namna ya utambulisho. Hii ni kwa sababu rangi ya sare ya jeshi hujulikana kote. Rangi ya sare ya jeshi hasa ya nchi yenye nembo ya simba ni ishara ya utawala na heshima kutoka kwa nchi zingine zilizowahi kutawaliwa na Uingereza Kwa hivyo maelezo haya yanaleta dhana ya utabaka kwamba kuna wanajeshi wa tabaka la juu na ambao wako juu ya sheria za nchi hasa walizozitawala na hawawezi kushtakiwa kwa kosa hata liwe la kuhuzunisha namna gani. Kisha kuna tabaka la mhadhiriwa wa maonevu ya mwanajeshi ambaye ni wa tabaka la chini, kwa kuwa hawezi kupata haki kwa maonevu anayotendewa na wanajeshi.

Katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 20), sehemu ya 13 ubeti 3,

Baada ya msimu wa ndoto tamu
Kuyoyoma na kufifia machoni
Bila dalili ya tarumbeta na vigelegele
Bila ishara ya ahadi tegemeki
Ndoto ya pete na tumba la viapo
Ilianza kupoteza ukijani-kibichi
Ikaingia umanjano ulikwajuka
Na kisha kijivu kama cha madakata

Mtunzi amesawiri jinsi matumaini ya binti anayegoja kuolewa yanavyokwajuka kwa kuyafananisha na rangi tofauti tofauti kama vile yanaanza yakiwa kijani kibichi. Kumaanisha kuwa binti ana matumaini yaliyodhabiti na baada ya muda yanaanza kupoteza ukijani kibichi na kuwa na umanjano kisha matumaini ya kupata mchumba yanapoishayanafananishwa na kijivu cha madakata. Mapito haya yote na mabadiliko ni usimbaji kwa kutumia hizi rangi. Rangi za matumaini kuanzia kijani kibichi, umanjano hadi kijivu ni ishara ya kuonyesha utegemezi wa mwanamke kwa mwanamume. Kuonyesha kuwa mwanamume ndiye anayeleta uhai (kijani kibichi) katika matumaini ya mwanamke. Kama atakosekana hivyo matumaini yanakufa na kuwa ya rangi ya kijivu (yasiyo na uhai).

### 3.2 Hitimisho

Katika kuonyesha majukumu yanayotekelezwa na rangi katika diwani hii ya *Rangi ya Anga,* mtunzi ameonyesha ufanisi wa kuegemea katika kusimba maana ya ujumbe wake na kumfanya msomaji kuwa na hamu ya kusoma zaidi ili kung'amua maana halisi ya ujumbe unaokusudiwa katika mashairi yote matatu. Kila shairi limetumia rangi kwa namna ya kipekee; Aidha kama ishara ya kuashiria ukweli wa uhalisia unaosimbwa.

Katika sura ifuatayo, tuliangazia mambo yanayomchochea mtunzi kufuata mkondo Fulani hasa wa rangi katika uandishi wake.

# SURA YA NNE
# RANGI KAMA KICHOCHEZI CHA MWANDISHI KATIKA DIWANI YA RANGI YA ANGA

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeangazia mambo yanayomchochea mtunzi kutumia mtindo fulani wa utunzi anapoandika kazi za kifasihi matumizi ya rangi katika kusimba maana ya kazi ya mashairi hasa mashairi huru kwa kutilia maanani maelezo yanayojitokeza katika Diwani ya Rangi ya Anga. Mtunzi wa kazi yoyote ya kifasihi hutoa msukumo wa kutunga kazi yake katika mazingira anamoishi kwa kuwa huingiliana na mazingira yake zaidi katika Maisha yake, mazingira ya mtunzi husheheni watu, Wanyama, jamii na tamaduni zao mbalimbali na matukio ya kila siku. Mtunzi wa kazi ya kifasihi huwa kama msanii anayechora picha fulani kwa kutumia rangi mbalimbali, hivyo kabla hajaanza kuchora hutayarisha vifaa vyake kwa kuteua rangi atakazozitumia kwenye mchoro wake au huwa kama mchongaji wa sanamu kwenye gogo au hata jiwe.

## 4.1 Mazingira

Mazingira huangaliwa kama chanzo au msingi wa uandishi wa mtunzi wa kazi yoyote ya kifasihi. Kwa hivyo mazingira, muktadha na historia huathiri maudhui ya mtunzi katika kazi yake ya kibunifu. Mambo haya matatu (mazingira, historia na muktadha) huweka msingi wa jinsi mtunzi atakavyoandika au kusema mambo fulani katika kazi yake (yaani fani atakazozitumia).

Katika uandishi wa kazi za kifasihi unachangiwa na mazingira ambayo yanamzunguka mtunzi wa kazi husika, mazingira ni muktadha unaodhibiti kitu au tukio fulani. Kuna miktadha ya aina mbili; muktadha finyu na muktadha mpana. Katika muktadha finyu huhusisha ulimwengu na hadithi yenyewe kwani wahusika, matukio ya hadithini, misimamo ya wahusika hudhibitiwa na mazingira ya wahusika hao katika ulimwengu wao wa kibunifu ilhali katika muktadha mpana, huhusu mazingira ya mwandishi kwani

kila mwandishi ni zao la jamii, tabaka, wakati na mtazamo fulani (Wamitila 2003). Hata hivyo mazingira ni kipengee ambacho hukosekana katika hadithi za kinjozi, hadithi za fantasia na hadithi za mazingaombwe.

Mandhari au mazingira ya mtunzi wa kazi ya kifasihi huweza kuchangia katika uandishi wake kwa kuwa hujumuisha eneo lake halisi la kijiografia au maelezo jinsi chumba, sehemu au mahali fulani palivyo. Mtunzi wa diwani teule amechochewa na mazingira ya Mto Thanantu, hasa katika shairi la *'Wanda'*ambao alishiriki kupiga mbizi na wenzake wa rika moja. Ameonyesha jinsi mto huo ulivyokuwa makaazi ya wanyama, ndege, samaki, wadudu na nyoyo za watu. Lakini sasa mazingira ya mto huo yamebadilika na anapoandika kifungu hiki anatumia kumbukumbu aliyonayo kuhusu enzi za mazingira mazuri. Kwa kuwa sasa mikono ya kilimo hasi chenye kuondoa mchanga na rutuba ya ardhi na kwato za wanyama wafugwao zimegofua na kurembua mazingira ya Mto Thanantu. Ni kutokana na mwingiliano wa mtunzi na mzingira yake kwani mtunzi ni kiumbe anayepatikana katika mzingira, wakati na mahali maalumu. Kwa mfano, katika sehemu ya 8 ya shairi la *'Wanda'* (uk 39), ubeti 4,

Moyo wangu unaungulika
Ewe tanuri ya simanzi!
Kwenye kingo changamfu za jana
Ambamo kwa rangi jamala
Njaa njaa
Ukoka
Na mianzi
Ilinawiri nyuso
Na miale
Mikindu
Na miringa
Kutabasamu
Na mitini
Migunga
Na mikoma
Kusimama kwa fahari,
Sasa magofu ya udongo

Yanadondokwa na huzuni

Katika ubeti huu mtunzi anatumia rangi jamala, ishara ya rangi nzuri ya mazingira ambayo yalikuwa yametawala katika Mto Thanantu. Rangi jamala imetumika kiusimbaji na mtunzi kuweza kufumba uzuri wa mazingira ya Mto Thanantu, ambao sasa uzuri wake umeharibika.

Maingiliano na watu pia huchangia jinsi mtu atakavyoandika kazi yake ya kifasihi. Maingiliano huleta utambulishaji hasa kupitia tamaduni za jamii husika. Kwa mfano, katika shairi la *'Rangi ya Anga'*, mtunzi amechora jamii za kufuga na tamaduni zao kama vile katika (uk 23), sehemu 15, ubeti 2 ,5;

Katika hii jamii ya sime na kanga
Baadhi ya ghulamu hukaguakagua mandhari
Na macho yanapotuama kwenye kidosho
Wanaibuka na mradi wa kuliwaza mwili
Kwa mtagusano nyerezi wa kimaumbile

Uwezo unapotimu mkononi
Barubaru huvumburuka hadi dukani
Na kujitwalia shanga za rangirangi
Chombo cha kumvusha kutoka jangwa
Hadi chemchemi za faraja teule

Mtunzi wa diwani hii ametambulisha jamii hii kama ya wenye kutumia sime na kanga. Vile vile amelinganisha jamii hii na kuwa hutumia shanga za rangirangi kuposea binti kwa wazazi wake. Kulingana na mwelekeo wa Charles Pierce katika nadharia ya semiotiki ni kwamba kila ishara huweza kuwa na maana zaidi ya moja. Kwa hivyo, shanga hizo za rangirangi ni ishara inayosimba mambo kadha kama vile, pingu za maisha, kunyimwa haki kwa mwanamke kuwa na mume mmoja, kwani akishaolewa huwa ni wa jamii nzima. Yaani mwanamke huyu hutumiwa na kila mwanamume katika jamii hii kama mke. Kwa hivyo shanga za rangirangi huwakilisha furaha kwa waume na huzuni kwa wanawake.

Kutokana na mwingiliano wa mtunzi wa diwani teule na watu wa jamii mbalimbali, ameona jinsi jamii tofauti tofauti zinavyounda tamaduni za kukandamiza jinsia moja hasa ya kike. Kwa mfano, katika shairi hilo hilo la *'Rangi ya Anga'*, (uk 3), sehemu ya 2, ubeti wa 2;

Kaida zenye kutu ya karne
Zimemkumbatisha nani
Haki ya kumiliki ardhi
Ambamo mikahawa nakawa
Na migomba na miparachichi
Inadarizi mandhari azizi
Kama zulia jamala
La kijani cha thamani?

Mtunzi ametumia maelezo haya kuonyesha jinsi mila na desturi zinavyomdhalilisha mwanamke kwa kumnyima haki za kurithi mali, matumizi ya maneno "zulia jamala la kijani cha thamani" ni ishara ya kusimba maana ya vitu vile vilivyonawiri na kustawi ndivyo mwanamke alivyonyimwa na jamii. Rangi ya kijani kama ilivyotumika katika muktadha huu ni ishara ya maana kuwa na uzuri au ubora.

Mtunzi anafananisha maji ya mvua na rangi nyekundu ambayo yanatiririka na kuhamisha uhai wa ardhi na kuacha mizizi nje. Maji mekundu ni ishara ya hatari, kwa kuwa jinsi udongo unavyobebwa na kuacha ardhi katika hali mbaya. Hii ni kwa sababu, rangi nyekundu huashiria hatari, hatari inayoletwa na kubebwa kwa mchanga na maji ya mvua ni kwamba mafuriko huja baadaye na madhara zaidi kwa binadamu na kusababisha kifo kwa binadamu na hata kwa wanyama. Kwa mfano, katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 42), sehemu ya 9, ubeti 3;

Vijia vyembamba!
Nyinyi
Wenye mivo mirefu,
Nyinyi
Udhia wa macho
Nyinyi

Matokeo ya ushirikiano bahili
Baina ya milolongo ya ng'ombe
Ikifukua ardhi kwa kwato,
Na maji mekundu yakitiririka
Na kuhamisha uhai wa ardhi
Na kuacha mizizi nje
Ishara ya majeraha buka

Wellek na Waren (1949) wanaeleza kuwa, fasihi hueleza jamii na kwamba fasihi ni zao la jamii ambalo huathiriwa na kuathiri jamii. Katika diwani hii ya *Rangi ya Anga*, mshairi kwenye shairi la *'Zimwi la Theluji'*, ameonyesha jinsi matukio katika jamii yalivyoathiri uandishi wake kwani ameeleza historia ya ujio wa ukoloni na athari zake kwa jamii nzima. Mtunzi ametoa mawazo yake katika matendo ya wakoloni na kuwachora kama waliokuja kuathiri jamii yake kwa namna hasi kwa kuchukua rasilmali za nchi kwa kutumia uongo, dini na elimu. Walipokabiliwa na Waafrika waliokuwa wamegundua njama zao waliwaua na kuzidisha idadi ya wajane na mayatima nchini. Katika sehemu ya (52), 4, ubeti 5;

Kwa ukungu wa hila
zimwi la theluji
liliapa kwa mbingu
na ardhi na nyota
kwa lilikuwa na dhima
ya wakala wa Mungu-
kuwahamasisha wenyeji
kutoka kichochoro kichafu
ambamo giza la dhambi
lilinguruma kama radi….

Matumizi ya rangi katika ubeti huu ni ya kihusishi kwani, neno giza lina maana ya rangi nyeusi. Rangi nyeusi kwa kawaida huhusishwa na mambo mabaya kama vile kifo, uchawi na uchafu. Katika muktadha huu, mtunzi wa diwani teule amesimba maana ya rangi nyeusi kama ishara ya uovu kwa kutumia giza.

## 4.2 Kutetea Haki za Wanawake

Mukobwa (1985), anasema kuwa vipawa vya utunzi hujidhihirisha kwa namna mbali mbali kwani kuna waandishi ambao huwa na lengo la kutafuta suluhu kwa matatizo yanayoikumba jamii yake na huwa na imani kwamba suluhu ya matatizo hayo inaweza kupatikana. Kuna kazi za kifasihi ambazo hulenga kuchochea jamii nzima ili kutatua matatizo yanayowakumba kwa kuhakikisha kuwa inawahimiza wanajamii kutafakari na kugundua suluhisho inayofaa. Mwandishi ambaye hulenga jambo hili katika kazi zake huwa ni wa kimapinduzi. Hulenga kuona jamii mpya inayowachochea watu kujikomboa na kujihimarisha. Haya yote ni kwa sababu, kila jambo litendekalo katika jamii huathiri wanajamii na mtunzi akiwa mmoja wa wanajamii huathirika vile vile. Mtunzi huonekana na wanajamii wenzake kama mmoja wao hata kama ni wa tabaka tofauti au ana nafasi tofauti katika jamii husika. Kwa hivyo mtunzi wa kazi za kifasihi hawezi kukwepa athari za jamii katika utunzi wake.

Katika kutetea haki za wanawake, mtunzi wa fasihi hudhamiria kuendeleza maisha kwa wakati wake. Hulenga kuwa kama kiwakilishi cha wakati wake na jamii yake. Kwa mfano, mtunzi anapaswa kuona hali halisi ya maisha ya jamii yake na kudhamiria kuleta mabadiliko ya mambo yanayodunisha jinsia moja au nyingine kwa kudhibitiwa na mifumo ya jamii husika. Mtunzi huzingatia mambo haya katika utunzi wake na kuhakikisha kuwa jamii imeathiriwa na utunzi wake.

Kwa mfano, katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 16), sehemu ya 11, ubeti wa 2;

…viti vya taadhima na uwezo
Vimepata wakaliaji wapya
Macho yao yanameta
Tofauti na sura zilizozoea,
Kwenye viti vya mawakili
Wengi waliokaa kwa kujiamini
Hawana dalili za masharubu
Bali videvu tembwere
Katika shoroba hospitalini
Na vyumba vya uchunguzi
Magwanda meupe pendezi

Yamepamba wenye marinda
Sawa na wenye shati na tai…

Mtunzi wa diwani hii amelenga kuonyesha uhalisia katika jamii yake jinsi mwanamke alivyofungwa na tamaduni zinazomtukuza mwanamume. Hata hivyo, mtunzi ameibadilisha hali hii katika ubeti ulio hapo juu kwa kuchora mwanamke aliyebadilika na kuchukua jukumu la kujitegemea kwa kusoma kufaulu na kufanya kazi yenye hadhi ya juu kama vile kuwa mtafiti, daktari, polisi na wakili. Matumizi ya maneno "magwanda meupe" yanayovaliwa na wanawake ni ishara inayosimba hali ya wanawake kuwa na uhakiki kwa wanayoyafanya pamoja na uaminifu. Mtunzi anapochora picha hii ya mwanamke katika akili ya msomaji ni matumaini yake kuwa jamii yake itabadilisha mwonoulimwengu wao kuhusu mwanamke na kumpa haki sawa na mwanamume.

**4.3 Kuibua Upekee / Ubunifu**

Kila mwandishi anapoandika kazi yake hukusudia kuwasilisha jambo jipya katika ulimwengu wa utunzi. Ni nadra na makosa, mtunzi wa kazi za kibunifu kutunga kazi zinazoiga utunzi wa awali wa watunzi wengine. Kila mtunzi huwa na lengo aidha la kuendeleza maarifa fulani au kujenga picha fulani kwa namna tofauti na jipya na hasa kuchangia kuleta maarifa mapya kwa binadamu katika uandishi wake. Mwandishi Kithaka wa Mberia, amekuwa na mchango mkubwa katika uandishi wa mashairi huru kwa kuyaandika kwa muundo wenye kuchora picha maalumu kuhusu hasa anachoandikia. Kwa mfano, katika diwani ya *Rangi ya Anga,* kwenye shairi la *'Rangi ya Anga,* ((uk 14), sehemu 10, ubeti 3;

Banati alipotimuliwa, alitimuka
Alipotimuka, aliteguka
Alipoteguka,
a
k
a
a
n
g

u
k
a
!

Mtunzi ameeleza jinsi msichana wa shule alivyofurushwa shuleni, na kuanguka kimaisha. Namna ya kuandika neno 'kuanguka' limeendelezwa jinsi mwendo wa kuanguka hufuata kutoka juu kwenda chini.

Katika shairi la *'Zimwi la Theluji'*, mtunzi ametumia neno LIPU! Katika (uk 56), sehemu 6, ubeti 3 na 4;

> Anga
> Lilitanda wekundu
> Na mitini
> Kulia bundi
>
> LIPU!
> Mwako ulilipuka!
> Mashujaa
> Wakauma midomo ya chini
> Na kukaza vipaji
> Kati ya visugudi
> Na mabega
> Misuli ilikakamka
> Na kutunisha vilimbili…

Neno hili "LIPU" ni ishara tanakali kulingana na Pierce katika mchango wake kwenye nadharia ya semiotiki, ambalo limetumika kuashiria jinsi Waafrika walivyojitolea kwa mlipuko mkali wa mashujaa ili kupigania haki yao iliyokuwa imechukuliwa na Wakoloni. Kutokana na hali iliyokuwa imejijenga ya ari ya kutaka kujikomboa kutoka kwa wakoloni, ndipo maelezo ya mtunzi yanaanza na kusema kwamba wekundu ulitanda angani. Hali ya wekundu ni ishara ya hatari iliyokuwa imewakabili Wakoloni

na Waafrika kwa kuwa na uwezekano wa umwagikaji wa damu. Matokeo ya vita hivi yalikuwa ni ongezeko la wajane na mayatima.

Katika baadhi ya vifungu katika diwani ya Rangi ya Anga, mtunzi ametumia majina ambayo ni ya lugha yake ya mama. Matumizi haya yanaweza kuchukuliwa kama namna ya mtunzi ya kuonyesha ufahari wake kwa jamii yake. Ama vile vile haya ni majina ya watu anaowaenzi katika jamii yake ikizingatiwa kuwa anaanza na mlezi wake, Kereka. Vinginevyo inaweza kuwa namna na nia ya kuleta msisitizo wa hali ya juu kwa msomaji.

Kwa mfano, katika shairi la *'Wanda'*, (uk 41) sehemu ya 9, ubeti 1;

Kibuhuti kinavuma mwangu moyoni-
Nakuhurumia, ewe Kereka
Mhisani uliyenilea,
Nawasikitikia, enyi Gitugu
Kwamwathu
Kamanyaki
Gaciongo
Gakauni
Kamaindi
Mutino
Nkarini
Ntoroni
Kamajagi
Ntumira
Na ahali yenu nzima
Kwa jinsi sura zenu
Zilivyojaa vidonda
Na damu mbichi

Mtunzi wa diwani hii ametumia mtindo huu ili kusisitiza ujumbe wake hasa kwa waathiriwa wa madhara ya uharibifu wa mazingira. Mtunzi anawaonya dhidi ya matokeo ya uharibifu wa mazingira kwamba umesababisha maafa na vifo. Maneno kama vile 'damu mbichi' ni ishara inayowakilisha matokeo halisi ya uharibifu wa

mazingira hii ni kwa sababu, damu huhusishwa na kifo na uhai vilevile. Rangi ya damu ni nyekundu kwa hivyo huashiria hatari, kifo na uhai.

**4.4 Kujaza Pengo la Kiusomi**

Vitabu vingi au bunilizi nyingi za kifasihi, vimeangazia mambo mbalimbali na kila mtunzi huwa anakazania na kulenga kuanzisha jambo jipya ambalo halijaandikiwa. Mtunzi wa diwani ya *Rangi ya Anga* ameangazia matumizi ya rangi ili kusimba maana ya ujumbe wake. Jambo hili la kutumia rangi, halijashughukiwa kwa kina na waandishi wengi katika fasihi andishi. Kila shairi katika diwani hii limetumia rangi kama ishara ya kusimba mambo mbali mbali. Kwa mfano, katika shairi la *'Rangi ya Anga'*(uk 20), sehemu ya 13 ubeti 3,

Baada ya msimu wa ndoto tamu
Kuyoyoma na kufifia machoni
Bila dalili ya tarumbeta na vigelegele
Bila ishara ya ahadi tegemeki
Ndoto ya pete na tumba la viapo
Ilianza kupoteza ukijani-kibichi
Ikaingia umanjano ulikwajuka
Na kisha kijivu kama cha madakata

Tukizingatia kwamba kulingana na Pierce katika nadharia ya semiotiki, ishara ni kitu kinachosimama mbadala wa kitu kingine. Rangi katika ubeti huu zimetumika kuwakilisha jambo jingine. Mtunzi ametumia rangi ya kijivu, kijani na manjano kusawiri mambo mbali mbali. Katika muktadha wa ubeti huu ameonyesha jinsi matumaini yanavyokwajuka na kuisha. Rangi ya kijani ni ishara ya matumiani ambayo yako imara kwamba linaloshikiliwa kutokea litakuja kutokea. Hali ya umanjano ni ishara kwamba matumaini yaliokuwa imara yameanza kuyeyuka na kupisha kutokuwa na uhakika. Kisha rangi ya kijivu cha madakata ni kukosa matumaini kabisa kwamba jambo litatokea.

Katika diwani tunaloshughulikia dhana ya rangi imetumika ili kujiepusha na kurudia yaliyowahi kuandikwa katika makala ya awali. Watunzi wengi wana anwani mbalimbalilakini anwani ya *Rangi ya Anga* imeandikwa pasi na kufanana na anwani

ingine yoyote. Hata hivyo mtunzi amedhihirisha matumizi ya rangi tofauti kwa kila suala. Kwa hivyo ni haki kusema kuwa diwani hii iliandikwa kwa msukumo wa kujaza pengo la kiusomi.

## 4.5 Kuzindua na Kutahadharisha Jamii

Moja ya dhima ya fasihi ni kuonya na kuchochea wanajamii kuhusu jambo ambalo linashusha hadhi ya jamii husika. Mambo mengi ambayo waandishi wengi huandikia huwa kwa nia ya kutuma ujumbe fulani kupitia kwa wasomi. Katika diwani ya *Rangi ya Anga*, mtunzi ametekeleza jukumu ili kwa kuonyesha jinsi waajiri wa wajakazi wa nyumbani wanavyowarai kwa kuwasifu na kuwapa zawadi na kisha kuwatunga mimba inayopelekea mama mwenye nyumba kuwafukuza na uja uzito wao. Kwa mfano, katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 18), sehemu ya 12, ubeti 6;

> Asubuhi ya kuraukia kazi ya mshahara
> Mlango wa nyumba ulipomwaga mama
> Baba aliyetangulia kuondoka nyumbani
> Hugeuza gari na kulielekeza lilikotoka
> Hadi nyumbani kwenye sumaku ya mwili
> Na kwa mawaridi mekundu ya maneno
> Kuanza kutunga koja nyerezi
> Akizungumzia siyo lishe ya watoto
> Sio unadhifu wa nyumba au nguo
> Bali akimshawishi mhudumu mchanga
> Waunde chombo cha kuchanganyia hisia
> Kiwainue kutoka sakafu ya utulivu chapwa
> Hadi anga la tufani za bashasha

Mtunzi ameonyesha jinsi bwana wa nyumba anavyomrai mjakazi wake kwa mawaridi mekundu ya maneno. Rangi nyekundu imetumika katika muktadha huu kuleta taswira ya hisia za mapenzi ya hatari. Japo rangi nyekundu ni rangi ya mapenzi, pia huwa ishara ya hatari na damu.

Kwa mfano, katika shairi la *'Zimwi la Theluji'*, mtunzi amekusudia kuwaonyesha wasomaji wake athari za ukoloni na madhara waliosababisha nchini huku akilenga kuwa, wasomaji wote wataweza kung'amua na kujua ukoloni mambo leo ambao upo katika nchi nyingi za bara Afrika. Waafrika hasa viongozi bado wanatukuza mkoloni kwa kuendeleza athari za ukoloni kwa watawaliwa. Kwa mfano, katika sehemu ya 5, ubeti wa 5;

Zimwi la theluji
Lilipokaza fundo
Kwa mikono imara
Lilichukua mitungi
Likavamia kiwele
Na kwa tamaa iliyokithiri
Kuanza kukamua maziwa
Na akiwa amechangamka
Kuyapakia katika vyombo
Na kwa tabasamu motomoto
Kuyasafirisha
Hadi ng'ambo

Zimwi la *t*heluji, ni ishara inayowakilisha ukoloni. Mtunzi ameeleza jinsi ukoloni ulivyokita mizizi barani Afrika na jinsi ukoloni ulivyochukua rasilmali za Afrika na kuzipeleka ng'ambo.

Katika kukashifu uozo unaokithiri katika jamii, mtunzi wa diwani hii na hasa katika shairi la *'Rangi ya Anga'* (uk 23), sehemu ya 15, ubeti 4 na 5;

Ombi linapendeza masikio masikivu
Bila banati kuulizwa msimamo
Bila kujali kama kibali cha wazazi
Kitaufanya moyo wake kuwaa kwa furaha
Au kufa ganzi kwa kumbo la majonzi
Ghulamu huanza mikakati kabambe
Kutafuta hadi kupata uwezo wa darahima

Kununulia shanga za rangiran

Uwezo unapotimu mikononi
Barubaru huvumburuka hadi dukani
Na kujitwalia shanga za rangirangi
Chombo cha kumvusha kutoka jangwa
Hadi chemchemi za faraja teule

Shanga za rangirangi zimesimbwa kuficha kuwa ni ishara ya uhuru kwa wanaume na ufungwa kwa wanawake. Mtunzi anatumia mfano wa tamaduni za jamii za ufugaji na kuhamahama na jinsi wanavyoposa na kumwoa mke kwa kutumia shanga za rangi rangi na kisha kumfanya kuwa mke wa kila mume katika jamii nzima. Kwa kutimizia kila mwanamume haja yake ya mapenzi. Kupitia kwa mfano huu mshairi anakusudia kujenga jamii mpya ambayo mwanamke anaheshimiwa na pia kuwatahadharisha wanajamii hawa dhidi ya madhara yanayoletwa na matendo yao ya kuwa na mke wa jamii nzima.

Katika shairi la *'Wanda'* (uk 44), sehemu ya 10 ubeti 5;

Tuiname
Tuokote jiwe
Tuinuke
Tulitupe mvoni-
Nia yetu adhimu
Kwenye huduma ya kwanza
Dhidi ya vidonda
Katika mwili wa mama
Nawaza, enyi sahibu,
Naota
Nawaotea miche adimu
Ya miti ambayo
Kwa ufasaha
Inazungumza Kitharaka
Na kuelewa hali ya anga

Na udongo,
Miti ambayo
Bila kukatishwa mdundo
Bila kuogopa gwakio za jua
Inaweza kucheza kwa ukunjufu
Katika ngoma ya kijani kibichi

Mtunzi ametekeleza jukumu hili la kuzindua wanajamii wa Wanda dhidi ya kukinga mazingira yao. Anawaita wenzake na kuwahimiza kupanda miche ili kurekebisha athari za matendo ya binadamu ya kukata miti na kubebwa kwa udongo. Mtunzi anawaonyesha taswira ya mazingira yenye miti ambayo imestawi na kuwa na rangi ya kijani kibichi. Rangi ya kijani kibichi katika muktadha huu inaashiria maumbile na ustawi.

**4.6 Hitimisho**

Uandishi wa kazi yoyote ya kifasihi lazima iwe imechochewa na jambo fulani kwani mtunzi aanzishi utunzi wake katika ombwe tupu. Vichochezi hivi huzuka kutoka mazingira ya mwandishi hadi mtunzi kuandika kwa nia ya kuziba pengo fulani la kiusomi. Ni muhimu kutambua kuwa mtunzi huyu ni wa kiume ilhali anatetea jinsia ya kike katika vitabu vyake vingi. Labda kulingana na mwono wake jinsia ya kike haina watetezi wa kiume wa kuzua athari anayowasilisha kupitia vitabu vyake na hivyo kuona pengo la kuingiza utunzi wake kwa kuzamia kufanya utafiti ili kuzindua watu kuhusu yanayomsibu mwanamke. Katika sura ifuatayo tulitoa muhtasari, mahitimisho na mapendekezo kuhusu kazi hii yote.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tunatoa muhtasari wa yote tuliyoyatafiti, mahitimisho tuliyoyapata na mapendekezo kwa tafiti zingine kuhusu kazi za kifasihi zinazojikita katika mada ya rangi kama mbinu ya usimbaji maana.

## 5.2 Muhtasari

Utafiti huu umechunguza matumizi ya rangi katika nyanja mbalimbali kama mbinu ya kuficha maana katika diwani ya *Rangi ya Anga.* Utafiti huu umeshughukia matumizi ya rangi katika maisha ya binadamu ya kila siku mpaka jinsi rangi ilivyochakatwa na kuwekwa katika uandishi hasa wa shairi huru. Katika diwani hii ya *Rangi ya Anga,* rangi imetumika kama ishara ya mikondo mbali mbali ya kijamii na vile vile imetumika kuonyesha majukumu yake katika diwani nzima.

## 5.3 Mapendekezo

Katika kazi hii tulitumia nadharia ya semiotiki inayochunguza matumizi ya ishara na uashiriaji kama kigezo cha kufumba ujumbe wa mwandishi hasa katika kazi za kifasihi na za kibunifu na hivyo kufikia mahitimisho kuwa mwandishi wa diwani ya *Rangi ya Anga* amepiga ndipo katika kufaulu katika kutumia rangi kama mbinu ya usimbaji.

Tunapendekeza kuwa tafiti za baadaye ziweze kutumia nadharia zingine kama vile nadharia ya uhalisia, upole na implikecha/umaanisho na zinginezo. Hizi nadharia zitawezesha kuona kama mtunzi wa diwani hii amefaulu kwa kiasi gani katika kutumia mbinu hii ya usimbaji maana kuwasilisha ujumbe wake. Vile vile, matumizi ya nadharia mseto yanaweza kutumika ili kuona namna ambavyo nadharia hizi zitashirikiana na kujalizana katika kutumia mbinu hii ya usimbaji na rangi kuwasilisha ujumbe wa Kithaka katika diwani ya *Rangi ya Anga.*

Mada hii ni imeshughulikiwa kwa namna ya kifasihi lakini inaweza kuchunguzwa kipragmatiki kwani dhana ya usimbaji ni ya kipragmatiki kwa hivyo napendekeza kuwa mada hii inaweza kushughulikiwa upya kwa kujikita zaidi katika pragmatiki ikizingatiwa kuwa taaluma nyingi siku hizi zinachukua mkabala wa umseto (interdisciplinary perspective) wa kitaaluma.

Katika kushughukia mada hii ya rangi kama mbinu ya usimbaji, tumekumbana na matatizo kama vile kukosa vitabu vya marejeleo kwa kuwa dhana ya kutumia rangi katika mbinu ya kusimba ujumbe ni mada ibuka na hivyo haijachunguzwa kwa kina na wataalamu hasa katika fasihi na isimu. Tunapendekeza kuwa tafiti za baadaye ziweze kushughulikia dhana kama za rangi, harufu na labda vipepeo kama zilivyotumika katika kusimba maana ya ujumbe wa kitabu kizima.

Diwani ya *Rangi ya Anga* ni kitabu kipya sokoni na hivyo napendekeza kifanyiwe tafiti zitakazochunguza mambo kama vile muundo, fani na maudhui kwa kuzingatia nadharia husika. Hata hivyo kwa kuwa diwani hii ni fupi ni itakuwa vyema zaidi kama itafanywa huku ikiunganshwa na diwani zenye miegemeo ya rangi kama diwani hii.

Nadharia ya semiotiki tuliyotumia tuliishughulikia katika mkondo uliopendekezwa na Charles Pierce na Ferdinand de Saussure, mpaka huu ulitukinga kuchunguza diwani hii katika mkondo wa Roland Barthes ambao umetumika na watafiti wengi kuchunguza kazi mbalimbali.

### 5.4 Hitimisho

Uchanganuzi wa rangi kama mbinu ya usimbaji maana ulihakikisha kuwa diwani ya *Rangi ya Anga* imesheheni ishara kama vile za ukoloni, umasikini, uovu, ustawi na hatari ambazo zinawakilishwa na rangi kama vile nyeupe, nyeusi, nyekundu, kijivu na kijani. Utafiti huu umedhihirisha kuwa maana za ishara zinatofautiana kulingana jamii husika, na kwamba maana za ishara hutambulika na wanajamii wanaolengwa.

## MAREJELEO


Abdalla, A. (1973). Sauti ya Dhiki. English press. Nairobi

Apopo, M. (2012*). Msimbo na maana katika tamthlia ya Zilizala.* Tasnifu yaM.A. Chuo kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)

Barthes, R. (1967). Elements of Semiology; London.

Chandler, D. (2002*). Semiotics: The Basics*. 2nd ed. London. Routledge

Cohan, S. & Shires, L. (1988*).* Telling Stories*: A theoretical Analysis of Narrative Fiction*. London & New York. Routledge

Griffen, R. (August,1997). Symbolic interactionism- based alternative. Makala kutoka www.sciencedirect.com

Karanja, M. (2014). Matumizi ya Istiara, Tasbihi na Taashira katika diwani ya Sauti ya Dhiki.Tasnifu ya M.A katika Chuo Kikuu cha Nairobi

Kilanga, S. (2014). *Ishara katika Kaptula la Marx* na *Kijiba cha Moyo*. Tasnifu ya M.A katika Chuo Kikuu cha Nairobi

Wa Mberia (2014). Rangi ya Anga. Nairobi. Marimba publishers

_________ (2002). Kifo Kisimani. Marimba publishers

__________ (2007). Natala. Nairobi. Marimba publishers

Msokile M. (1993). Msingi wa Uhakiki wa Fasihi. Nairobi. East Africa Publishers

Mulila, J. (2009). *Usawiri chanya wa wahusika wa kike katika tamthlia ya Zilizala na Chamchela*. Tasnifu ya M.A. chuo kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa)

Muthoni, M. (2014). *Maudhui na Mtindo katika Tikitimaji*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)

Nyanchama, B. (2004). Matumizi ya taswira na ishara katika sauti ya dhiki. Tasnifu ya M.A katika chuo kikuu cha Kenyatta (haijachapishwa)

publishers

Sauder, L. (2012, October 25) *The Maasai Tribe of Kenya.* Makala kutoka http:/www.prezi.com

Senkoro, F.E.M.K. (1988*).* Ushairi*, Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam. University press

Too, M. (2011). *Uchanganuzi wa kifasihi wa baadhi ya fani katika Nguso Mama*. Tasnifu ya M.A Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Umberto Eco, (1976). A Theory of Semiotics. London. Macmillan publishers

Wafula, R. & Kimani, N. (2007). *Kiswahili na Elimu nchini Kenya*. Nairobi. Kolbe press

Walibora, K. & Said, A. (2007). Damu Nyeusi na Hadithi nyingine. Nairobi. Macmillan publishers

Wamitila, K.W. (2002). Uhakiki wa Fasihi. Nairobi. Focus publishers

_____________ (2003). Kamusi ya Fasihi: *misingi na vipengele vyake*. Nairobi. Focus publishers

_____________ (2007). Msimu wa Vipepeo.Nairobi. Vide Muwa

_____________. (2008). Kanzi ya Fasihi: *misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi. Vide Muwa publishers

____________ (2012). Harufu ya Mapera. Nairobi. Vide Muwa

Wanyonyi. B. (2011). *Uhakiki wa riwaya ya Nyuso za Mwanamke*. Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi